Rufiji Environment Management Project[1]

**Environmental Management and Biodiversity Conservation of Forests, Woodlands, and Wetlands of the Rufiji Delta and Floodplain**

# Taarifa Ya Warsha Ya "Ujirani Mwema Na Rufiji" Iliyofanyika Tarehe 3 Hadi 4 Desemba 2002, Ikwiriri, Rufiji

# Proceedings of the "Good Neighbours with Rufiji" workshop held on December 3rd and 4th at Ikwiriri, RUFIJI (Contains a summary in English)

**Bukwali, J., Hogan, A.R., Chande, M.S., Elibariki, R., Eniyoye, J., Chirwa, E.**



**Technical Report No. 34**
**April 2003**

**For more information please contact**

**Project Manager,**
Rufiji Environment Management Project,
P.O. Box 13513,
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel. 44 Utete Rufiji or 023-2402972/022-2666088,
Mobile 0741-322366 Dar es Salaam
Email: rempute1@bushmail.net or iucndar@epiq.or.tz

[1] [1]The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN-The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy

## Rufiji Environment Management Project – REMP

**Project Goal:** To promote the long-term conservation through 'wise use' of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced**.**

**Objectives**

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.
- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.
- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

**Project Area**

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

**Project Implementation**

The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.

Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

**Project Outputs**

At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:

An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners.

# Muhtasari


**Warsha Ya Ujirani Mwema Na Wilaya Rufiji**

Wilaya ya Rufiji inaandaa mpango bora wa usimamizi wa mazingira. Wilaya imetambua kwamba ushirikiano mzuri na wilaya za jirani ni muhimu kuweza kufaulu katika utekelezaji wa mpango huu. Kwa hiyo wilaya, kwa kutumia uwezeshaji wa Mshauri wa Maliasili wa Mkoa, ilikaribisha wilaya na taasisi za hifadhi za jirani kutafakari kwa pamoja suala la usimamizi wa mazingira.

Warsha hii iliyofanyika kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 03/12/2002 hadi tarehe 4/12/2002 ilifunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mheshimiwa Nicodemus M. Banduka na kuhudhuriwa na washiriki mbalimbali ikiwa ni pamoja na waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, wawakilishi wa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya pamoja na wataalamu kutoka Idara za Ardhi Maliasili na Mazingira katika Wilaya za Mafia, Rufiji, Mkuranga na Kisarawe. Washiriki wengine ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira wa Wilaya ya Rufiji, wawakilishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Wizara ya Malisili na Utalii.

Lengo la warsha lilikuwa ni kuandaa mbinu za pamoja katika kutatua matatizo yanayokwamisha juhudi za wilaya katika kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Ili kufikia lengo madhumuni ya warsha yalijumuisha pamoja na:

- Kuwapa watumishi wa wilaya jirani nafasi ya kukutana na kufahamiana vizuri.
- Kupeana taarifa ili kufahamu maliasili zilizopo wilaya nyingine, kufahamu miradi ya usimamizi wa maliasili na mahusiano yake na wilaya na kuelewa mikakati ya wilaya husika dhidi ya matumizi haribifu.
- Kuchambua masuala yenye utata na mbinu za kuyatatua.
- Kuunda mbinu za pamoja katika kutatua matatizo yahusianayo na usimamizi wa maliasili.
- Kujadili jinsia na mahusiano yake katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.
- Kutafuta mbinu za kuboresha mawasiliano kama kuwa na mtandao wa mawasiliano.

Kwa ujumla madhumuni ya warsha yalikuwa sambamba na matarajio ya wanawarsha.

Wajumbe wa warsha waliwasilisha taarifa za wilaya na taasisi wanakotoka. Taarifa hizi zilitolewa na wataalam wa idara za halmashauri, taasisi mbalimbali pamoja na wanavijiji kutoka vijiji vya mfano katika mradi wa MUMARU. Kila taarifa ilijadiliwa kwa kina, maswali kuulizwa, majibu kutolewa, pamoja na michango mingine ya maoni na ufafanuzi. Pamoja na uwasilishaji wa mada wanawarsha waligawanywa katika vikundi vitano vilivyoshughulikia matatizo ya uvujaji wa maliasili (wanyamapori, misitu, samaki), mipaka na mawasiliano. Mgawanyo huu ulizingatia utaalamu wa mwanawarsha kisekta katika vitengo vya wanyamapori, misitu, ardhi na uvuvi. Suala la mawasiliano lilishughulikiwa na maafisa maliasili wa wilaya. Baada ya mawasilisho na majadiliano, zoezi hili lilifuatiwa na wajumbe kurudi tena katika vikundi vyao ambapo kila kikundi kilipendekeza mikakati ya kudhibiti uvujaji wa maliasili kutokana na matatizo yaliyokuwa yameorodheshwa katika majadiliano ya awali. Baada ya zoezi hili kila kikundi kilichagua tatizo moja walililoiona ni kubwa na kupendekeza mikakati na njia (jinsi) ya kutekeleza mikakati hiyo. Mapendekezo ya kila kundi yaliwasilishwa na mjumbe mmoja kutoka kila kundi. Wajumbe wote walichangia mawazo mbalimbali kwa nia ya kuboresha.

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika michango ya wajumbe ni pamoja na:

- Wilaya kuwa na maliasili mbalimbali ikiwa ni pamoja na misitu, bahari, na mazao ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kamba fukwe, nyuki, na maeneo ya mambo ya kale.

- Sehemu kubwa ya maliasili hizi zimekuwa zikitegemewa na serikali kuu pamoja na serikali za halmashauri ya wilaya kama vyanzo vikuu vya mapato. Utegemezi huu mkubwa umekuwa ni chanzo cha uvunaji usiozingatia uwiano kati ya mavuno na hali halisi ya maliasili husika, jambo ambalo linahatarisha kuwepo kwa maliasili hizo na kusababisha uharibifu wa mazingira
- Pamoja na uvunaji huo halmashauri za wilaya hazifaidiki sana kutokana na sehemu kubwa ya mapato kupelekwa serikali kuu na kutoroshwa kupitia njia zisizo rasmi**.**

Baada ya mawasilisho na michango mbalimbali wanawarsha walitoa maazimio kama ifuatavyo:

1. Suala la mipaka hasa kati ya wilaya na wilaya na kati ya wilaya na hifadhi, lipewe kipaumbele badala ya kusubiri migogoro kutokea.
2. Mipango ya usimamizi bora ya ardhi na malisili iandaliwe kwa lengo la matumizi endelevu.
3. Wananchi wawezeshwe na mamlaka za wilaya kusimamia vizuri maliasili zote zinazowazunguka.
4. Doria za pamoja (kati ya wilaya na wilaya) kwenye maeneo ya uvunaji wa maliasili mipakani, ziimarishwe.
5. Utafiti ufanyike ili kujua hali halisi ya raslimali zilizopo ili kuweka viwango vya uvunaji wenye uwiano.
6. Utaratibu madhubuti wa ukusanyaji mapato yatokanayo na uvunaji kamba uandaliwe ili kuwezesha serikali, halmashauri na vijiji kupata mapato stahili.
7. Asilimia kubwa ya mapato yanayokusanywa kutokana na mazao ya maliasili yabakie wilayani kuendeleza shughuli za uhifadhi.
8. Utafiti ufanyike kwenye eneo linalodhaniwa kuwa ni mazalia ya kamba ambalo lipo kusini mwa Bwejuu (Kijiwe Nyara) hadi Kilwa ili uthibitishwe na hatimaye lihifadhiwe.
9. Wafugaji wadogo wa samaki na kamba wahamasishwe na kuendelezwa na Halmashauri za wilaya ili kuboresha kipato chao katika suala zima la kupiga vita umasikini.
10. Kila Halmashauri ya wilaya itayarishe orodha ya raslimali zilizopo kwenye wilaya yake ili kuandaa mpango madhubuti wa uhifadhi na matumizi endelevu wa raslimali hizo.

Pamoja na maazimio, wanawarsha walitoa tathmini iliyoonyesha kufanikiwa kwa lengo la warsha. Warsha hii ilifungwa rasmi na ndugu J.K. Bukwali, Afisa Maliasili Mshauri katika Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani ambaye pia alikuwa mwezeshaji katika warsha. Alimshukuru mwandaaji ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya (Idara ya Ardhi Malisaili na Mazingira), Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira (MUMARU) na IUCN kwa kuwezesha kuwepo kwa warsha iliyoongeza uelewa wa matatizo ya uhifadhi miongoni mwa watendaji na njia za kuyakabili. Aidha aliwataka wajumbe kutekeleza yale yaliyoazimiwa ambayo yapo ndani ya uwezo wao na kuandaa mkakati wa kushirikisha wahisani/wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Mashirika ya Kiserikali na yasiyo ya kiserikali katika kutekeleza yale yanayohitaji msaada wa aina hiyo.

# Summary

Rufiji District Council, with the technical assistance of IUCN is in the process of making and implementing an environment management plan. The District realizes that in order for the plan to work effectively it needs to cooperate closely with the management of neighbouring districts and nature reserves. Therefore the Rufiji district Council, with the facilitation of the Regional Natural Resources Officer, invited forty-five of its neighbours to deliberate on the issues involved in sustainable management of its natural resources at a "Good Neighbours of Rufiji" Workshop.

The workshop was held at FDC, Ikwiriri on December 3rd and 4th and was officiated by the Regional Commissioners and representatives of district Executive Directors from Mafia, Kisarawe, Mkuranga and Rufiji districts; Department and sectoral heads from the Natural Resources and Lands departments of those districts; representatives of Mafia Island Marine Park, Jaja, Twasalie, Mbunjumvuleni and Mtanzamsona Village Environment Management committees, the National Mangrove Management Project, WWF, the Ministry of Natural Resources and Tourism and the National Environment management Council. Unfortunately representatives of Kilwa district Council and Selous Game Reserve did not attend.

The goal of the workshop was to: **Devise ways to jointly solve the problems which limit the effectiveness of Rufiji district's efforts to sustainably manage its natural resources.** The specific focus was the "leakage of natural resources", that is, the illegal removal of natural resources across district borders and the ways to control this movement.

The workshop aims were to:

- Provide an opportunity for district personnel to meet and get to know each other
- Exchange information regarding the natural resources present in each district, the efforts being made to manage them and the problems being encountered.
- Discuss the problems and analyse opportunities and solutions.
- Devise joint strategies for improving natural resource management
- Discuss gender roles in environment management
- Identify means of improving communications between district neighbours.

The goal and aims were compatible with the expectations of the participants who came prepared with their presentations on the types and extent of their natural resources, methods, routes and the estimated levels of leakages of the resources. The presenters, from district natural resources department, villages, WWF and Mafia Island Marine Park also described the means in operation at present for controlling the harvest and movement of natural resources. They also described the difficulties and the reasons why they are encountered. The subsequent discussions, which were very lively, yielded further information and produced and extensive list of detailed problems. By working in small groups, created according to sectoral lines, recommendations were made regarding ways to tackle the problems caused by ill-defined boundaries and by weak inter-district. Communication problems were tackled by multidisciplinary groups. The recommendations of each group were presented to the plenary and challenged and improved during a question and answer session. The groups then prioritised their solutions and made detailed action plans and budgets for implementing the most important solutions. These action plans and budgets were presented to the plenary and following further discussions the following resolutions were made.

1. The issue of boundary clarification, especially between districts and districts and the Selous
2. Game Reserve should be given top priority. It should be done before conflicts occur.

3. District should prepare land and natural resource management plans to enhance sustainable utilization.
4. 3. Communities should be facilitated by district authorities to manage the natural resources which surround them.
5. Joint patrols, in areas of natural resources harvest on the boundaries, should be established and strengthened.
6. Research should be done to establish the present and the sustainable rates of the natural resources especially fish, prawns, forests and wildlife.
7. The system of revenue collection from prawn harvests to improve benefits to villages and the district should be established.
8. The income sharing mechanism should be put in place whereby large proportion of revenue generated from natural resources should be retained by the districts for use towards improved management of those resources.
9. Research should be carried out in the area between Bwejuu, Kijiwe Nyara, and Kilwa to check the species and productivity of the prawn nursery there which may need to be protected.
10. Small scale fish and prawn farming should be supported and promoted to enhance community income generating capacity as one of the strategy towards poverty alleviation.
11. Good neighbours workshop should be held at least once per years.
12. Every district should prepare and maintain an inventory of all of her natural resources so as to enhance both their conservation and sustainable utilisation.

The workshop was evaluated by the participants who gave very positive feedback especially on the level of participation and the topic focus of the proceedings. Special praise was given to the village representatives for their knowledge and commitment to sustainable management of their natural resources. The regional Natural Resources Advisor, Mr. Bukwali, closed the workshop by thanking the participants for their well-prepared presentations and for their active involvement in the groupwork and discussions. He expressed a hope that some of the actions proposed could be funded internally by districts, but suggested that the proposers should also seek funding from the central government and appropriate donors for their practical and sensible suggestions. He thanked Rufiji district council and especially the District Lands, natural resources, and Environment Office for providing the secretariat and the logistical support for this very useful event. He thanked REMP/IUCN for the technical and material support which, through this workshop, has given him an enhanced opportunity to understand and advise on the ground-level natural resources management problems in the Region.

# Yaliyomo

**Muhtasari** ... i
**Summary** ... iii
**Majedwali** ... v
**Vifupisho vya maneno** ... vi
**1 Sehemu Ya Kwanza** ... 1
1.1 Utangulizi ... 1
1.2 Ufunguzi wa Warsha ... 1
1.3 Kujitambulisha ... 1
1.4 Lengo na madhumuni ya warsha ... 2
1.5 Kanuni za warsha ya ujirani mwema ... 2
1.6 Mada zilizotolewa na wilaya, taasisi mbalimbali na vijiji vya mfano ... 2
**2 Sehemu Ya Pili** ... 13
2.1 Mgawanyo wa wanawarsha kwenye vikundi ... 13
2.2 Kazi za vikundi ... 13
2.3 Mawasilisho ya vikundi ... 13
2.4 Kazi ya pili ya vikundi ... 16
**3 Sehemu Ya Tatu** ... 17
3.1 Muhtasari wa mada mbalimbali zilizowasilishwa kwenye warsha ... 17
3.2 Tathmini ya warsha ... 18
3.3 Maazimio ya warsha ... 20
3.4 Kufunga Warsha ... 20
**4 Viambatisho** ... 21
4.1 Kiambatisho Namba 1: Ratiba Ya Warsha ... 21
4.2 Kiambatisho Namba 2: Washiriki wa warsha ... 22
4.3 Kiambatisho Namba. 3: Hotuba ya Mgeni Rasmi ... 24
4.4 Kiambatisho Namba. 4: Sekta Ya Uvuvi Wilaya Ya Rufiji ... 26
4.5 Kiambatisho Namba 5: Uvunaji Wa Mazao Ya Misitu Kutoka Wilaya Ya Rufiji Na Kusafirishwa Wilaya Jirani ... 29
4.6 Kiambatisho Namba 6: Taarifa Ya Idara Ya Maliasili Wanyamapori Wa Ya Rufiji ... 31
4.7 Kiambatisho Namba 7: Halmashauri Ya Wilaya Ya Mkuranga ... 33
4.8 Kiambatisho Namba 8: Maelezo Mafupi Kuhusiana Shughuli za Hifadhi ya Bahari Mafia (MIMP) ... 35
4.9 Kiambatisho Namba 9: Mafia District Council Description of Mafia Natural Resources Utilisation ... 37
4.10 Kiambatisho Namba 10: A Brief Presentation on Leakage of Natural Resources (Mangroves) ... 41
4.11 Kiambatisho Namba 11: Taarifa Ya Wilaya Ya Kisarawe ... 46
4.12 Kiambatisho Namba 12: Maelezo Ya Wilaya Ya Kisarawe Kuhusu Utoroshaji Wa Mazao YaMisitu Na Wanyama Kutoka Kisarawe ... 49

# Majedwali

Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Taarifa ya uvujaji wa maliasili katika wilaya ... 11
Jedwali Na. 2: Mawasilisho ya matatizo na mapendekezo ya ufumbuzi. ... 13
Jedwali Na. 3: Mawasilisho Ya Vikundi ... 16
Jedwali Na. 4: Muhtasari: Tathmini Ya Washiriki na Warsha ... 19

# Vifupisho vya maneno

| Kifupisho | Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|---|
| CBC | Ushirikishwaji wa jamii katika shughuli za Uhifadhi | Community Based Conservation |
| CBNRM | Ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa maliasili | Community based Natural Resources Management |
| DLNREO | Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira wa Wilaya | District Lands Natural Resources and Environment Officer |
| CEAS | Mpango wa tuzo ya kuhifadhi mazingira Pwani | Coastal Environment Award Scheme |
| FDC | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi | Folk Development College |
| FR | Msitu wa Hifadhi | Forest Reserve |
| GTZ | Shirika la Msaada wa Maendeleo la Ujerumani | German Technical Aid |
| HAT | Chama cha Wawindaji Tanzania | Hunters Association of Tanzania |
| ICM | Usimamizi wa Uwiano wa Mazingira ya Pwani | Intergrated Coastal Management |
| IUCN | Muungano wa Kimataifa wa Kuhifadhi Mazingira | International Union for Conservation of Nature and Natural Resources/World Conservation Union |
| JFM | Usimamizi Shirikishi wa Misitu | Joint Forest Management |
| KDU/APU | Kikosi dhidi ya Ujangiri | Antipoaching Unit |
| MIMP/HIBAMA | Hifadhi ya Bahari Mafia | Mafia Island Marine Park |
| MMP | Mradi wa Taifa wa Mikoko | Mangrove Management Project |
| MUMARU/ REMP | Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji | Rufiji Environment Management Project |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | National Environment Management Council |
| PRA | Tathmini Shirikishi ya Vijiji | Participatory Rural Appraisal |
| RNRA | Afisa Maliasili Mshauri wa Mkoa | Regional Natural Resources Advisor |
| SGR | Pori la Akiba la Selous | Selous Game Reserve |
| TCMP | Ushirkiano wa Usimamizi wa Pwani ya Tanzania | Tanzania Coastal Management Partnership |
| TFCG | Kikundi cha Uhifadhi wa Misitu Tanzania | Tanzania Forest Conservation Group |
| VEO | Afisa Mtendaji wa Kijiji | Village Executive Officer |
| VHF | Masafa Marefu Zaidi | Very High Frequency |
| VNRCS | Kamati za maliasili za Vijiji | Village Natural Resources Committees |
| WCST | Chama cha Uhifadhi wa Maliasili Tanzania | Wildlife Conservation society of Tanzania |
| WEO | Afisa Mtendaji wa Kata | Ward Executive Officer |
| WMA | Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori | Wildlife Management Areas |

# 1 Sehemu Ya Kwanza

## 1.1 Utangulizi

Warsha hii iliyofanyika kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 3-4/12/2003 katika ukumbi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Rufiji (Rufiji FDC) ilihudhuriwa na wajumbe 45 kati ya wajumbe 55 walioalikwa. Kwa bahati mbaya wajumbe kutoka wilaya ya Kilwa na Pori la Akiba la Selous hawakuweza kuhudhuria.

## 1.2 Ufunguzi wa Warsha

Akitoa hotuba yake wakati wa ufunguzi, mgeni rasmi Mheshimiwa Nicodemus M. Banduka, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, aliainisha sababu kubwa mbili za usimamizi duni wa maliasili. Alizitaja sababu hizo kuwa za kiuchumi kwa upande mmoja na kiutawala kwa upande wa pili.

Kwa upande wa eneo la kiuchumi alitaja uthamini usio sahihi na uhitaji wa mapato ya haraka kama chanzo cha uharibifu. Kwa upande wa utawala aliutaja uwezo mdogo wa halmashauri za wilaya kuwa chanzo cha usimamizi duni.

Kutokana na kasoro hizo aliainisha kuwa halmashauri za wilaya hukusanya asimilia 10 tu ya mapato kutokana na mazao ya maliasili na kuacha asimilia 90 kuibiwa, jambo linalosababisha hasara kubwa kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla. Alisikitishwa na kushangazwa na wilaya kuwa na utajiri wa maliasili wakati Halmashauri na wananchi wote wakiishi kwenye dimbwi la umasikini. Hata hivyo alionyesha faraja aliyopata kutoka kwa baadhi ya wilaya kuanza kuchukua hatua za kubadilisha hali hiyo, Rufiji ikiwa ni mojawapo. Alitaarifu kuwa kwa kipindi cha miaka minne, mradi wa Usimamizi wa Mazingira kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya umebadilisha mtazamo kwa kufanya utafiti na kufahamu kiwango cha uharibifu na upotevu wa mazao ya maliasili ikiwa ni pamoja na misitu, wanyamapori na mazingira kwa ujumla. Aidha wamejenga mwamko wa wadau wa ngazi zote kuthamini na kujadili matumizi endelevu ya maliasili na mazingira, vilevile wamejenga uwezo wa wahusika kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya katika kutengeneza mipango ya uhifadhi na matumizi endelevu na utekelezaji wake. Kwa kuzingatia ukweli kuwa wilaya moja haiwezi kudhibiti udhaifu aliouongea peke yake alipongeza wilaya ya Rufiji kwa kuona umuhimu wa kuwaita majirani kwa lengo la kufahamiana, kubadilishana uzoefu na kujenga mawasiliano mazuri ili kuandaa mkakati wa pamoja wa kusimamia vizuri maliasili. Alionyesha matumaini yake ya warsha kutoa maazimio madhubuti yatakayosaidia katika usimamizi na matumizi endelevu katika wilaya zote. Kwa maelezo zaidi ya hotuba ya mgeni rasmi, angalia Kiambatisho namba 3.

## 1.3 Kujitambulisha

Madhumuni yalikuwa ni kufahamiana kwa njia ya kuchangamshana na kupata maoni ya washiriki kuhusu hali ya maliasili na mazingira nchini. Wanawarsha waliombwa kutafuta sura ngeni ukumbuni na kuhojiana maswali matatu ikiwa ni pamoja na kufahamu jina la mhusika, cheo chake na anavyoona hali ya mazingira. Wengi walionyesha masikitiko yao ya maliasili kuvunwa kupita uwezo wake na kusisitiza haja ya kuzitunza maliasili zilizopo vizuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Baadhi ya semi zilizojitokeza ni pamoja na "mazingira yanaharibika", "uvuvi wa meli kubwa unasababisha uharibifu", "uvunaji wa misitu na uchomaji mkaa umekithiri", "uchomaji moto ovyo na uvunaji holela unasababisha uharibifu wa mazingira", kasi ya uharibifu wa mazingira ni kubwa mno", "uhifadhi wa mazingira sio endelevu", "maliasili tunayo lakini mazingira yanaharibika", "mazingira yanaonyesha dalili ya kuendelea vizuri", mazingira haya yaendelezwe ipasavyo kuchangia uchumi wa Taifa", "hadhi ya mazingira inarudi vizuri", "wananchi wameanza kuelewa na hali itakuwa nzuri", na "hali ni mbaya misitu inakatwa ovyo".

## 1.4 Lengo na madhumuni ya warsha

Wazo la kuwa na warsha lilitokana na ushauri wa mkoa na mradi wa MUMARU, kutokana na matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza ikiwa ni pamoja na:-

- Migongano juu ya uhalali wa umiliki wa mazao ya maliasili kama vile
- Maeneo ya uvunaji wa mazao ya misitu na wanyamapori
- Usahihi wa viwango vinavyotumika kuhalalisha kiasi cha mazao yanayovunwa
- Nyaraka zisizo sahihi wakati wa kusafirisha mazao kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Sababu zilizofanya Rufiji kuchaguliwa kuandaa warsha ni juhudi za uhifadhi zinazoonyeshwa na wilaya ambazo zinaweza kuigwa na wilaya nyingine katika kuimarisha shughuli za ulinzi na matumizi endelevu ya maliasili.

Lengo la warsha lilikuwa ni kuandaa mbinu za pamoja katika kutatua matatizo yanayokwamisha juhudi za wilaya katika kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.

- Madhumuni ya warsha yalikuwa ni pamoja na:

- Kutoa nafasi kwa watumishi wa wilaya zinazopakana kufahamiana na hivyo kuimarisha nafasi ya mawasiliano kiutendaji.
- Kupeana taarifa juu ya maliasili zilizopo katika wilaya nyingine, kufahamu miradi ya usimamizi wa maliasili na mahusiano yake na wilaya na kuelewa mikakati ya wilaya husika dhidi ya matumizi haribifu.
- Kuchambua masuala yenye utata na mbinu za kuyatatua.
- Kuunda mbinu za pamoja katika kutatua matatizo mbalimbali ya uhifadhi
- Kujadili jinsia na mahusiano yake katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili
- Kutafuta mbinu za kuboresha mawasiliano kwa mtandao.
- Kupeana taarifa ili kufahamu maliasili zilizopo wilaya nyingine, kufahamu miradi ya usimamizi wa maliasili na mahusiano yake na wilaya na kuelewa mikakati ya wilaya husika dhidi ya matumizi haribifu.
- Kuunda mbinu za pamoja katika kutatua matatizo yahusianayo na usimamizi wa maliasili.

## 1.5 Kanuni za warsha ya ujirani mwema

Katika kuhakikisha kuwa warsha inafanikiwa kanuni za kuendesha warsha ziliandaliwa na kukubaliwa na washiriki ikiwa ni pamoja na:

1. Uhuru wa kutoa mawazo.
2. Kumpa kila mshiriki nafasi ya kusikilizwa wakati wa kuchangia.
3. Kujali muda.
4. Kuwa na juhudi za kuchangia ili kufanikisha warsha.
5. Kuepusha kauli zinazoweza kutafsiriwa kuwa na dalili za ubaguzi wa kijinsia.
6. Kutumia lugha ya kiswahili ili kuwezesha ushiriki mzuri wa wanawarsha wote.

## 1.6 Mada zilizotolewa na wilaya, taasisi mbalimbali na vijiji vya mfano

Katika kuwasilisha taarifa za shughuli za uhifadhi, ulinzi na matumizi ya maliasili, wilaya ya Rufiji kutokana na kuwa mwenyeji, ilipewa upendeleo kwa Afisa Ardhi Maliasili na Mazingira na wasaidizi wake ambao ni wakuu wa vitengo mbalimbali kila mmoja wao kutoa mada. Kwa upande wa wilaya nyingine, ni Maafisa Maliasili wa Wilaya tu waliotoa mada.

## MUHTASARI WA MADA MBALIMBALI

### 1.6.1 Idara ya Maliasili na Mazingira-Wilaya ya Rufiji

Mtoa mada Ndungu M.S. Chande Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira alieleza shughuli zinazofanywa na wilaya katika kusimamia mazingira. Aliwafahamisha wanawarsha kuwa kwa kushirikiana na Mradi wa Uhifadhi Mazingira Rufiji (MUMARU) ambao unaandaa mpango wa muda mrefu wa usimamizi wa mazingira ambao utaingizwa katika mpango wa maendeleo wa wilaya wameweza kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:- Kufanya utafiti juu ya maliasili zilizopo ili kuzifahamu na kuziwekea mikakati ya usimamizi.

- Kutengeneza mipango ya usimamizi wa mazingira ya vijiji (VEMP) na kuunda kamati za mazingira za vijijij.
- Kujenga ufahamu wa wadau juu ya masuala ya mazingira.
- Kujenga uwezo wa wadau juu ya masuala ya mazingira.
- Kujenga uwezo wa watumishi wa wilaya na wadau wengine kwa njia ya mafunzo mbalimbali katika kusimamia mazingira.

Aidha mtoa mada alieleza mafanikio yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na:-

- Kuandaliwa kwa taarifa mbalimbali kutokana na tafiti zilizofanyika katika nyanja za misitu, uvuvi, wanyamapori, uchumi wa vijiji, tathmini ya thamani ya maliasili, n.k.
- Kukamilika kwa mipango ya usimamizi wa mazingira katika vijiji vinne vya mfano. Vijiji hivyo vina kamati hai za maliasili/mazingira.
- Wadau wengi kufahamu masuala ya usimamizi wa mazingira.

Kufanikiwa kwa sherehe ya siku ya mazingira duniani iliyoadhimishwa kimkoa wilayani Rufiji mjini Ikwiriri mwaka 2000 na iliyoadhimishwa kiwilaya katika kijiji cha Kikale mwaka 2001 ni ishara ya kuongezeka kwa ufahamu wa wadau wa masuala ya uhifadhi.

- Kutolewa kwa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa wilaya ndani na nje ya nchi ambayo yamewajengea uwezo wa kusimamia mazingira
- Kuanzishwa kwa miradi ya ufugaji nyuki, uoteshaji na upandaji miti na kilimo cha miche ya matunda na mboga kwenye vijiji mbalimbali.

### 1.6.2 Mada kutoka kitengo cha Uvuvi Rufiji

Katika mada yake, Afisa uvuvi wa Wilaya Ndugu E.B. Chirwa aliitaja Bahari ya Hindi kama raslimali kubwa ambayo huiwezesha wilaya kuvuna samaki wenye uzito wa tani 3,500 ambazo huingiza dola za Marekani 800,000 (Tshs. 800 mil.) kwa mwaka. Alieleza pia kwamba Kamba ni kati ya samaki wanaovuliwa na kusafirishwa na kusindikwa viwandani ambapo wavuvi wadogo huzalisha tani 2200 zenye thamani ya dola milioni 4 kwa mwaka. Aliwafahamisha wanawarsha kuwa 80% ya Kamba wanaovuliwa na meli hutoka delta ya Rufiji. Mambo mengine aliyoyagusia kwenye mada ni pamoja na:-

1. Matumizi haribifu (uchafuzi wa mazingira) ya bahari ambao husababishwa na kumwagwa kwa takataka, mafuta, mabaki ya samaki, na uchafu wa binadamu, jambo ambalo husababisha kushuka kwa ubora na wingi wa kamba na pia kuhatarisha afya za binadamu.
2. Uvuvi wa meli ambao husababisha kupunguza uwezo wa bahari kusimamia viumbe mbalimbali.

Kutokana na matatizo hayo alishauri mambo ya kufanya ikiwa ni pamoja na:

- Kufanya utafiti wa madhara ya uvuvi wa meli (Trawling) na hatimaye kuchukua hatua stahili.

- Kuwepo uvuvi mbadala.
- Kupunguzwa kwa idadi ya leseni; na
- Kufupishwa kwa muda wa msimu wa uvuvi.

Mtoa mada alizungumzia pia masuala yenye utata ikiwa ni pamoja na:

1. Uhakiki usio mzuri wa kiwango kinachokusanywa na viwanda jambo linalosababisha Halmashauri kukosa ushuru.
2. Tofauti za ushuru baina ya wilaya jirani.

Aidha aliyataja matatizo yanayokabili kitengo cha uvuvi ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha (ufinyu wa bajeti) na vitendea kazi. Alishauri uboreshaji wa bajeti katika kitengo cha uvuvi na kutengewa fedha kutoka wizarani (Retention) kutokana na ushuru wa kamba. Mada iliyotolewa imeambatishwa kama kiambatisho Na. 4.

Baada ya mada michango mbalimbali ilitolewa ikiwa ni pamoja na:

1. Utafiti wa kitaifa wa kamba ili kuandaa viwango stahili vya kuvunwa.
2. Kutokuwepo kwa takwimu sahihi jambo ambalo linasababisha Halmashauri kutofahamu kiwango stahili cha ushuru. Mfano kampuni ya Tanpesca huipatia halmashauri ya wilaya ya Rufiji Shs.2m kila mwezi bila kuwa na vigezo vya kutoa fedha hiyo.
3. Malalamiko ya wananchi kwa idara ya uvuvi kuwa na upendeleo kwa kuwaruhusu wageni kutumia kokoro huku watanzania wakikatazwa.
4. Ushauri wa kuboreshwa kwa ukusanyaji ushuru kutokana na kamba kwa kuwa na utaratibu mzuri wa kujua kiasi cha kamba kinachokusanywa toka katika maeneo mbalimbali ya wilaya.
5. Ushauri wa kuchukua hatua stahili kuzuia maafa yanayoweza kusababishwa na athari za uchafuzi wa mazingira kutokana na usindikaji.
6. MUMARU kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wananchi katika suala la ufugaji
7. Haja ya Wataalam wa uvuvi kutembelea Mafia kuona nini kiwanda cha Tanpesca kinafanya kuhusiana na ufugaji wa samaki aina ya tasi kwenye matundu (cages).
8. Kuhimiza viwanda vya samaki kufuata utaratibu wa sheria.
9. Wataalamu wa uvuvi wawezeshwe na wilaya kufanya kazi zao k.m kukusanya takwimu, ugani, ushirikishwaji wa jamii na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria.

### 1.6.3 Mada kutoka kitengo cha misitu Rufiji

Mtoa mada Bw. Minde, Afisa Misitu wa Wilaya, alizungumzia utoroshaji na usafirishaji wa mazao ya misitu nje ya wilaya ambao umekuwa wa muda mrefu. Alionyesha ramani aliyochora ya njia hizo za usafirishaji wa mazao hayo ambayo ni pamoja na mbao, mkaa na kongowele. Aliyataja maeneo yanayohusika kuwa Mtita, Mchungu, Mtanzamsona na Ruhoi. Aidha alizungumzia wavunaji kutofuata utaratibu na sheria ambapo alitoa mfano wa mbao 300 na magogo vilivyokamatwa vikitoroshwa nje ya wilaya. Alizitajwa njia zinazotumika kutoroshea mazao ya misitu ambazo ni barabara na Bahari. Alitaja hatua zilizochukuliwa na wilaya kudhibiti uvunaji holela ikiwa ni pamoja na kusimamia sheria mama, kuongeza doria, kuandaa na kutumia sheria ndogo, ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia maliasili za misitu, uanzishaji wa misitu ya vijiji na kamati za mazingira na ushirikiano na miradi mbalimbali iliyopo wilayani. Pamoja na kutaja hatua za udhibiti, alitaja pia mfanikio ikiwa ni pamoja na kupungua kwa kasi ya uharibifu na utoroshwaji, uanzishaji mipango ya ushirikishwaji kwenye vijiji vya mfano vya mradi, mpango unaotegemewa kusambazwa wilaya nzima. Aliwafahamishwa pia

wajumbe kuwa sekta ya misitu iliweza kuchangia shs. Milioni 26 katika mapato ya halmashauri ya wilaya na shilingi milioni 14 upande wa serikali kuu kwa mwezi Novemba, 2002. Alieleza pia matatizo yanayosababisha kushindwa kudhibiti uvunaji ambayo ni kutoelemika kwa jamii, kutoeleweka kwa mipaka, kutokuwepo utaratibu wa mawasiliano, uhaba wa wataalamu, ucheleweshaji wa fedha za retention kwa ajili ya doria, kuwepo kwa barabara zisio rasmi, umasikini na kukosekana kwa ajira mbadala jambo linalofanya jamii kushiriki kwenye uvunaji holela. Kwa maelezo ya kina angalia Kiambatisho namba 5 cha mada iliyotolewa.

Katika majadiliano wajumbe walisisitiza haja ya kufuata utaratibu wakati wa kushughulikia suala la mipaka kwani ni la kitaifa ambapo ngazi mbalimbali za kulitatua zinafahamika. Walielekeza lawama kwa viongozi kwa kutoitikia wito wa vikao vya usuluhishi wanapoalikwa. Aidha walishauri uchambuzi wa utumiaji wa wadau wote wakati wa kushughulikia suala la mipaka ili kuwa na suluhisho la kudumu.

### 1.6.4 Mada kutoka kitengo cha Wanyamapori, Rufiji

Mtoa mada Bw. Eniyoye, John-Afisa Wanyamapori wa Wilaya aliwafahamisha wanawarsha juu ya uhifadhi wanyamapori unaofanyika katika vijiji vya Ngarambe, Tapika, Mtanzamsona, Mloka na maeneo mengine. Aidha alizitaja taasisi zinazojihusisha na uhifadhi wa wanyamapori ikiwa ni pamoja na WWF, shirika la uhifadhi wa mazingiza duniani (IUCN), Shirika la ushirkiano la Ujerumani linalojihusisha na mradi wa ushirikishwaji wananchi katika matumizi endelevu ya wanyamapori pembezoni mwa Pori la akiba la Selous (GTZ), Mradi wa Usimamizi wa Mazingiara Rufiji (REMP) unaofadhiliwa na Serikali ya Uholanzi kupitia shirika la uhifadhi ulimwenguni (IUCN). Mtoa mada aliainisha pia faida za wilaya kupakana na Selous ambazo hutokana na uwindaji wa kitalii ambapo wilaya hupata asilimia 25 ya mapato ambayo ni sawa sawa na Shs.12m hadi 15m kwa mwaka. Pia alitaja kijiji cha Ngarambe ambacho hupata sh.5.6m kwa mwaka licha ya kitoweo kwa wananchi. Kijiji cha Tapika ambacho kimepakana na Selous pia hupata shs.300,000/= hadi 400,000/= kwa mwaka. Uwindaji wa wananchi kwa ajili yakitoweo huchangia shs. 3m hadi 4m kwa mwaka. Kwa upande wa uvujaji alitaja nyara na kitoweo pamoja na njia zinazotumika katika kutoroshea mazao hayo. Aidha alielezea ukataji leseni katika wilaya ya jirani (Kisarawe) na kuwindia Rufiji kuwa jambo linalokosesha Halmashauri mapato na ni suala ambalo limekuwa likileta migongano kati ya wilaya husika. Katika kudhibiti mianya ya uvujaji alieleza hatua zinazochukuliwa ikiwa ni pamoja ushirikiano na taasisi zisizo za kiserikali na serikali katika kuanzisha uhifadhi uliokitwa katika jamii, doria za pamoja kwa ushirikiano na Selous na kikosi cha kuzuia ujangili, mkakati wa kuanzisha hifadhi za wanyama za vijiji (WMA), kusaidia vijiji katika kutunga sheria ndogondogo za vijiji, kuwa na walinzi wa wanyampori katika vijiji na uimarishaji wa vizuia vya maliasili. Pamoja na udhibiti, mtoa mada alitoa mikakati mbalimbali inayotarajiwa kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori ikiwa ni pamoja na:

1. Kushirikisha pande zote zinazohusika katika migogoro ya mipaka.
2. Kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori.
3. Kuimarisha doria.
4. Kueneza elimu yauhifadhi wa wanyamapori vyuoni na mashuleni.

Mtoa mada alimalizia kwa kushauri kutengewa fedha zaidi kwa lengo la kuimarisha kitengo chake na kuongeza motisha kwa watumishi. Pia alishauri kutafuta wafadhili kwa kuwa rasilimali ya wanyamapori sio ya wilaya tu bali taifa na mataifa. Mada yake imeambatishwa kama kiambatisho na. 6. Katika kuchangia, mwanawarsha mmoja alilaumu halmashauri kwa kutotenga fedha za kutosha kwa shughuli za wanyamapori. Alitoa mfano wa kutofanyika kwa doria za mara kwa mara jambo lililosababisha Tembo kuuawa karibu na makao makuu ya wilaya mwaka jana mwezi Julai. Aidha mwanawarsha mwingine alishauri halmashauri kuanglia uwezekano wa kupata ushuru toka kambi za kitalii.

### 1.6.5 Mada kutoka wilaya ya Mkuranga

Mtoa mada, Bw. M. Kinana-Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira wa Wilaya, alianza kwa kuelezea kwa ufupi namna wilaya ya Mkuranga inavyotegemewa na wafanya biashara wa mazao ya maliasili kutoka Dar es Salaam, pia inavyojitahidi kukabiliana na uharibifu wa maliasili kwa kushirikisha wadau mbalimbali kutoka nje na ndani ya wilaya. Aliezea kuwa shughuli za ukusanyaji ushuru wa halmashauri kutokana na mazao ya maliasili (misitu na samaki) hushughulikiwa na mawakala. Aidha taarifa yake iligusia mambo yanayochangia katika uvujaji wa maliasili mbalimbali ikiwa ni pamoja na maingiliano ya kikazi, kiidara na kiwizara, ukosefu wa fedha na vitendea kazi, mgawanyo wa mapato kutokana na maliasili na migogoro ya mipaka.

Alitaja mikakati ya wilaya yake dhidi ya uharibifu wa maliasili kuwa ni kupitia semina na warsha mbalimbali, kupeana taarifa za kikazi, doria za pamoja, kutoa taarifa maalumu hasa za utoroshaji wa maliasili kwa wilaya na taasisi husika na utoaji wa motisha. Pia utaratibu wa mashindano ya shughuli za uhifadihi mazingira kwa wilaya na wilaya. Aidha alipendekeza ushirikishwaji wa wadau wa jinsia zote, akina mama kupewa msamaha wa kulipia leseni za utandaji wa samaki baharini, uanzishaji wa kijarida cha shughuli za mazingira/uhifadhi na kubadilishana taarifa za uhifadhi mazingira kati ya wilaya na wilaya ama mikakati ya uboreshaji uhifadhi. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatisho Na. 7.

### 1.6.6 Mada kutoka Hifadhi ya Bahari Mafia

Mtoa mada, G.S.A. Melele, Mhifadhi katika Hifadhi ya Bahari Mafia (HIBAMA) alianza na maelezo mafupi kuhusiana na shughuli za hifadhi ya bahari ambayo ilianzishwa kwa lengo la kuhifadhi raslimali za bahari kwa matumizi endelevu. Alieleza kuwa hifadhi lilianzishwa mwaka 1995 kwa sheria Namba 29 ya mwaka 1994. Hifadhi hii ina vijiji 11, katika visiwa vidogo vya Chole, Jibondo, Juani na Bwejuu. Aliyataja pia madhumuni ya hifadhi kuwa ni pamoja na:

1. Kulinda na kuhifadhi.
2. Kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo.
3. Kukarabati mifumo ya ikolojia iliyoharibika.
4. Kuwashirikisha wadau wa hifadhi ya bahari katika mipango ya maendeleo ya uhifadhi na matumizi endelevu.
5. Kuchangia matumizi ya rasilimali ambazo hazijatumika k.m. chaza na kaza.
6. Kuhifadhi na kulinda makumbusho ya kihistoria na kitamaduni.

Alieleza pia muundo wa utawala wa HIBAMA kuwa uko chini ya bodi ya wadhamini katika ngazi ya taifa, kamati ya ushauri katika ngazi ya wilaya na kamati za hifadhi za vijiji. Alizitaja rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na

- viumbe mbalimbali wa bahari;
- misitu ya aina tano za mikoko, msitu wa Mlola; na
- fukwe.

Alieleza changamoto ya hifadhi ya bahari Mafia kuwa matumizi ya nyavu za kuvuta na zenye macho madogo, msongamano wa wavuvi wahamiaji, na uchomaji moto ovyo, uvunaji wa matumbawe, ukataji miti kiholela na uanzishwaji wa viwanda vya kusindika samaki.

Alibainisha pia hatua zilizochukuliwa kuwa ni pamoja na:

- Elimu ya mazingira kwa jamii;
- Kuendesha doria;
- Kukagua maeneo ya matumizi katika kanda;

- Kuanzisha mpango wa kubadilishana mitego, yaani kuchukua ile haribifu na kuwapa wavuvi mitego endelevu; na
- Kubuni njia mbadala za kiuchumi kama kilimo cha mwani, ufugaji wa nyuki, samaki, kilimo cha mazao ya biashara mfano Korosho na Alizeti. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatisho namba 8.

### 1.6.7 Mada kutoka wilaya ya Mafia

Mtoa mada Ndugu I. Mtani, Mwakilishi wa Afisa Maliasili wa Wilaya alianza kwa kuelezea jiografia ya wilaya ambapo aliwafahamisha wanawarsha kuwa wilaya ipo Mashariki mwa Pwani ya Tanzania km. 160 kutoka Dar es Salaam na ina ukubwa wa kilomita za mraba 518. Alieleza pia kuwa wilaya hiyo inaundwa na visiwa vinane, visiwa vikubwa vinne vikiwa ni makazi ya watu, wakati visiwa vingine vinne ni kambi za uvuvi. Aidha aliainisha maliasili zilizopo wilayani ikiwa ni pamoja na msitu wa hifadhi wa Mlola wenye ukubwa wa hekta 125.2 unaomilikiwa kwa pamoja na taasisi mbili ambazo ni Halmashauri ya wilaya (Hekta 50.2), na Hifadhi ya Bahari Mafia (Hekta 75), msitu wa mikoko wenye ukubwa wa hekta 4,045 na misitu ya jamii ambayo ni kilombero, Mwamizi na Jimbo.

Pamoja na misitu alitaja pia bahari ambayo ina utajiri wa bioanuwai wakiwemo samaki, Nyangumi, Kasa, Kamba, Mwani, Matumbawe n.k. Alihusisha utajiri huo na uanzishaji wa Hifadhi ya kwanza ya Bahari nchini, Hifadhi ya Bahari Mafia (HIBAMA). Alibainisha uvuvi kuwa shughuli muhimu na ya pili kiuchumi baada ya kilimo ambayo huwaingizia wavuvi wadogo wadogo pato kubwa. Alitoa takwimu kuwa mwaka 1999 Mafia ilikuwa na wavuvi 3194, vyombo vya uvuvi 688 na walivuliwa samaki tani 58000.72 wenye thamani ya shs. 728.400.000. Alizitaja zana zilizotumika kuwa ndoano 1022, nyavu 699, mitego 1076, majarife 495 na nyavu za kuingiza 8.

Licha ya mazao ya bahari alibainisha pia kuwepo kwa maliasili nyingine ikiwa ni pamoja na wanyamapori kama vile Viboko, Digidigi, Nyani, Nguruwe, Nyoka, na ndege wa aina mbalimbali. Maliasili nyingine ni Nyuki na Kumbukumbu za mambo ya kale. Aidha alizitaja taasisi mbalimbali zinazoshirikiana na wilaya katika shughuli za uhifadhi ambazo ni Hifadhi ya Bahari Mafia (HIBAMA), Seatrust/WWF na NORAD katika uhifadhi wa kasa, nguva na mikoko.

Kwa upande wa masuala yenye utata alitaja maeneo mawili ambayo ni mipaka na udhaifu katika usimamizi. Aligusia pia matatizo ya msingi yanayoikabili wilaya katika uhifadhi wa maliasili ikiwa ni pamoja na:

- uhaba wa boti;
- gharamza za uendeshaji wa vyombo hivyo;
- uvunaji usio endelevu kwa kutumia zana hafifu;
- ukataji miti ya asili;
- uharibifu wa sehemu za mazalia ya samaki km. Ndege, popo, matumbawe, na mayai ya kasa;
- mipaka ya kijiografia inayosababisha gharama kubwa za uendeshaji;
- mawasiliano yasiyoaminika; na
- hali duni ya wananchi licha ya kuzungukwa na utajiri wa maliasili.

Katika kutatua matatizo hayo alipendekeza ushirikishwaji wa wadau katika mipango na ufuatiliaji wake na kuimarisha elimu ya ufahamu kwa kuwaeleza wananchi kujiunga kwenye vikundi/ushirika ili kupata mikopo yenye unafuu. Aliiomba wizara ya Maliasili kuona umuhimu wa kuipa wilaya ya Mafia fedha za "Rentention" . Pamoja na hayo aligusia suala la jinsia ambapo alionyesha ushiriki wa kuridhisha wa akina mama katika shughuli mbalimbali za maliasili. Kwa upande wa shughuli

zinazoweza kufanywa kwa pamoja na wilaya jirani alishauri uanzishwaji wa majarida ya kanda, matumizi ya luninga na radio, ubadilishanaji wa taarifa za utendaji na uandaaji wa mikutano, warsha, na semina za pamoja. Mada aliyoitoa imeambatishwa kama kiambatisho Namba 9.

### 1.6.8 Mada kutoka Mradi wa Mikoko Kanda ya Kati

Mtoa mada Ndugu Frank Sima, Afisa Mikoko, aliwafahamisha wanawarsha kuwa Mradi wa Uhifadhi Mikoko upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, katika Idara ya Misitu na Nyuki na una lengo la kuongeza mchango wa mikoko katika pato la taifa kwa kuhimiza matumizi endelevu. Alifahamisha kuwa mradi umekuwa ukiendeshwa kwa awamu ya miaka minne minne ambayo ni 1994-1998, 1998-2002, na ya sasa 2002-2006. Alieleza kuwa Ukanda wa Pwani ambapo mikoko hustawi una urefu wa km 800 kutoka mpakani mwa nchi ya Kenya hadi kusini katika nchi ya Msumbiji. Alitoa takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii za mwaka 1989 ambazo zilionyesha kuwa misitu ya mikoko Tanzania bara ina ukubwa wa hekta 115,000. Kati ya hizo, hekta 53200 zinapatikana katika delta ya Rufiji wilayani Rufiji sawa na asilimia 46 ya misitu yote ya mikoko Tanzania bara. Urefu wa delta ni km 65 na wastani wa upana wa km 25. Kiutawala alieleza kuwa maeneo ya mikoko yamegawanywa katika kanda tatu ikiwa ni pamoja na:

- Kanda ya kaskazini ambayo ipo katika Mkoa wa Tanga
- Kanda ya kati ambayo inajumuisha wilaya za Bagamoyo, Dar es Salaam, Mkuranga na Rufiji; na
- Kanda ya kusini inayohusisha Lindi na Mtwara.

Akielezea njia za uvujaji; mtoa mada alizigawanya katika makundi manne ikiwa ni pamoja na utoroshwaji wa miti ya mikoko unaofanywa na wananchi katika vijiji vya delta na kuisafirisha katika maeneo ya Mafia, Dar es Salaam, Zanzibar, n.k; uvunaji unaofanywa na wafanyabishara kutoka nje ya wilaya ya Rufiji na kusafirisha mazao ya mikoko hadi Mafia, Zanzibar na maeneo mengine; wafanyabishara wenye leseni halali wanaobeba zaidi ya kile walichoruhusiwa; na uvunaji haramu unaosababishwa na migongano ya mipaka baina ya wilaya ya Rufiji na wilaya nyingine.

Katika kuthibiti uvunaji: Mtoa mada alieleza hatua zilizochukuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha kamati za maliasili za vijiji katika vijiji 24 kupitia mikutano mikuu ya vijiji ambapo Mradi ulitayarisha mwongozo wa uanzishaji wa kamati hizo. Shughuli ambazo zimekuwa zikifanywa na kamati hizo ni pamoja na: Doria, ufuatiliaji wa sheria, uandishi wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu, shughuli za ugani kwa jamii nzima ya kijiji, utoaji wa taarifa za uhalifu na upandaji miti. Hatua hizo zimeongeza pamoja na mambo mengine shughuli za ugani mashuleni, uoteshaji wa ukuzaji na miti ya mikoko na usimamizi wa uvunaji.

Alitaja hatua nyingine zilizochukuliwa kuwa ni uendeshaji wa semina za kuimarisha ukusanyaji ushuru, jambo ambalo limeboresha viwango vya ushuru unaokusanywa na Halmshauri ya wilaya kwa mfano kijiji cha Kwale kiliweza kukusanya shilingi 660,000 kutoka kwenye vyombo 20 vya majini mwezi Juni 2002, baada ya semina ikilinganishwa na shilingi 147,000 zilizokusanywa mwezi April, 2002 kabla ya semina.

Mtoa mada aligusia pia matatizo ambayo Mradi umekuwa ukiyapata katika shughuli za uhifadhi ikiwa ni pamoja na utumiaji wa misumeno ya umeme, unaoharibu mazingira ya mikoko katika kijiji cha Pombwe unaofanywa na wavunaji kutoka Kilwa. Mahusiano ya kiukoo ya wananchi wa Mafia na Rufiji ambapo baadhi ya watu wanavuna katika sehemu zote mbili, jambo ambalo linasababisha uvushaji kutoka Rufiji hadi Mafia. Alishauri ushirikiano wa dhati kati ya maafisa kutoka pande zote mbili.

Aidha aliielezea wilaya ya Mkuranga kuwa njia mojawapo ya usafirishaji wa mazao ya mikoko kuelekea Zanzibar na Dar es Salaam. Alihimiza maafisa maliasili wa wilaya kuhakikisha kuwa

wafanyabiashara wana vibali vyote vya kijiji, wilaya na serikali kuu kutoka wilayani Rufiji. Alishauri pia uimarishaji wa usimamizi katika vizuia vya Mkuranga kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa ushuru wa halmashauri na Taifa. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatisho Namba, 10.

Wakitoa mchango wao wanawarsha walionyesha udhaifu wa mradi kutokuwa karibu na watumishi wa maliasili wilayani. Walishauri ushirikishwaji wa karibu zaidi.

### 1.6.9 Mada kutoka vijiji vya mfano vya Mradi wa MUMARU

Wawakilishi wa vijiji vya mfano vya mradi wa MUMARU walielezea uzoefu wao katika usimamizi wa mazingira katika vijiji vyao. Wawakilishi hao wanne walitoka katika kamati za usimamizi wa mazingira na vijiji vya mfano. Watoa mada walikuwa wanne (Twasalie, Jaja, Mvuleni na Mtanzamsona) na walitoa mada mbili moja ya vijiji vya delta vya Twasalie na Jaja na nyingine ya vijiji vya tambarare ya mafuriko vya Mtanzamsona na Mbunjumvuleni.

**Mtanzamsona na Mbunjumvuleni-Tambarare za Mafuriko**
Watoa mada Ismail Lusonzo, Mwenyekiti wa kamati ya Mazingira kijiji cha Mtanzamsona akisaidiana na Amina Kiambwe, mjumbe wa Kamati ya Mazingira - Mbunjumvuleni walieleza hatua walizopitia katika mchakato wa kuweza kumiliki na kusimamia maliasili zilizopo kijijini mwao. Walieleza kuwa vijiji vya Mtanzamsona na Mbunjumvuleni ni miongoni mwa vijiji vya mfano ambayo vina mipango yake ya usimamizi wa mazingira. Mipango hiyo imetokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili hapo awali ya kutofaidika kutokana na maliasili zinazowazunguka. Aidha waligusia malengo/madhumuni ya kijiji ambayo ni kurudishia rasilimali zote zilizotoweka, kuhakikisha maliasili inatumika kwa busara, Kuwa na mbinu mbadala za uchumi ambazo zitalinda misitu na mazingira kwa ujumla, kuhakikisha kuwa maliasili za misitu, samaki na wanyamapori zinasimamiwa ipasavyo na kuwa takwimu sahihi za maliasili na kupewa uwezo kwa kushirikishwa katika kusimamia misitu.

Walieleza pia mikakati iliyofanyika na inayoendelea kutekelezwa kuwa ni pamoja na:-

- kutenga eneo la msitu wa kijiji kwa kuweka alama katika mipaka ya msitu huo;
- kuimarisha doria, hasa katika msitu wa kijiji;
- kuanzisha kambi ya ulinzi ndani ya msitu wa kijiji;
- kueneza elimu ya uhifadhi kijijini, katani, tarafa hadi wilayani;
- kuwa na mahusiano mema; na
- kufanya tafiti mbalimbali.

Watoa mada waliyataja pia mafanikio waliyoyapata tangu walipopata elimu ya uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na ufugaji nyuki, upandaji miti, ukamataji mbao uliowapatia shilingi 27,000 kama zawadi ya kijiji kwa kutoa taarifa na kushiriki kwenye doria, kupungua kwa uvunaji holela wa misitu, ufahamu mkubwa wa wanakijiji juu ya suala la uhifadhi mazingira na utaalamu wa kilimo cha mboga na matunda ambayo yanaendelea kutafutiwa masoko.

Pamoja na mafanikio waligusia pia matatizo mbalimbali yanayowakabili kama vile ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kutoka Idara ya Maliasili, migogoro ya mipaka na ukosefu wa nyenzo za kutosha katika kuboresha kazi za ulinzi wa msitu na wanyamapori.

Watoa mada pia waliiomba wilaya ya Kisarawe kuwaruhusu na kuwawezesha wananchi wa vijiji vya Vikumburu na Kitonga kufanya mikutano ya ujirani mwema na Mtanzamsona, kushawishi kijiji cha Kitonga kuwa na mpango wa ushirikishwaji jamii katika usimamizi wa maliasili. Vilevile walishauri kumaliza suala la mgogoro wa mpaka kati ya Kisarawe na Rufiji na kuwa na doria za pamoja baina ya wilaya husika kwa kushirikiana na kijiji cha Mtanzamsona.

Mwisho walinukuuu tamko la sera ya misitu linaloainisha misitu ya vijiji kusimamiwa na serikali za vijiji ama vyombo vingine vilivyochaguliwa na serikali za vijiji kwa lengo la kulinda vyanzo vya mali kwa kuzingatia madhumuni na mipango ya usimamizi.

**Vijiji vya Twasalie na Jaja**
Mtoa mada Mzee Koge, Mwenyekiti wa kamati ya mazingira alieleza kuwa Twasalie ni kijiji cha asili kilichoandikishwa na ni kati ya vijiji vya mfano vya MUMARU. Alieleza kuwa kijiji hicho kina eneo kubwa la kilimo ukilinganisha na vijiji vingine na Wana mpango wa kupata na kutumia trekta la mkopo kutokana na ahadi ya Mkuu wa Wilaya. Vile vile kina utajiri wa maliasili za aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na misitu ya mikoko, wanyamapori na samaki. Aliongeza kuwa wanayo pia majangwa ya chumvi. Kwa upande wa shughuli za uhifadhi alieleza kuwa wanakijiji wameunda vikundi ambavyo vimepata mafunzo mbalimbali na kupatiwa vifaa kwa ajili ya shughuli binafsi na za kijiji. Aidha wamekwisha tenga maeneo kwa matumizi mbalimbali yakiwemo yale ya usimamizi shirikishi wa misitu kwa kushirikiana na Idara ya Misitu na Nyuki. Kwa upande wa kijiji cha Jaja ndugu Athumani Ally alionyesha kutototofautiana kwa malengo na shughuli zinazofanywa na kijiji cha Twasalie ila alionyesha kusikitishwa kwake na matumizi haribifu ya mikoko yanayofanywa na wafanyabiashara kwa kutozingia viwango vya ukubwa wa miti na utoroshaji maliasili ya mazao ya mikoko. Aliainisha hatua walizochukua katika kukabiliana na matatizo hayo kwa kusimamia uvunaji na ukaguzi wa mikoko.

### 1.6.10 Mada kutoka Wilaya ya Kisarawe

Mtoa mada alielezea matatizo, maeneo ya utoroshaji wa maliasili na hatua ambazo wilaya imezichukua kukabiliana na matatizo hayo. Aidha mtoa mada aliwashitua wajumbe kwa kutaja kuwa watoroshaji wengine hutorosheza maliasili katika wilaya ya Rufiji. Kwa maelezo zaidi angalia viambatisho namba 11 na 12.

### 1.6.11 Mada kutoka Programu ya Uhifadhi Kanda ya Kaskazini Mashariki Pori la Akiba Selous.

Mtoa mada Ndugu Cyprian Malima aligusia historia ya mfuko wa uhifadhi ulimwenguni (WWF) ambapo aliwafahamisha washiriki wa warsha kuwa shughuli za mfuko huo zilianza nchini mwaka 1965 ambapo mpaka wakati huu unatekeleza miradi 10. Aidha mtoa mada alieleza shughuli zinazofanywa chini ya mfuko huo katika kudhibiti utoroshwaji wa maliasili ikiwa ni pamoja na Elimu ya mazingira kwa umma, ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi wa maliasili na kuwasaidia wananchi kubuni njia mbadala za uchumi ili kupunguza utegemezi wa maliasili.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Taarifa ya uvujaji wa maliasili katika wilaya**

| **Aina ya Maliasili inayovuja/ Inayotoroshwa** | **Maeneo Husika** | **Hatua za kudhibiti** | **Matatizo yanayojitokeza** | **Njia za kusaidiana kudhibiti** |
|---|---|---|---|---|
| RUFIJI:<br>Mazao: Misitu<br>-Magogo<br>-Mbao<br>-Boriti<br>Wanyapori:<br>-Nyara<br>-Kitoweo<br>Maliasili za Uvuvi:<br>-Kamba<br>-Samaki | -Mloka Vikumburu<br><br>-Mchungu Delta<br>-Pombwe<br>-Kibanju<br>-Salale | -Kuimarisha doria<br><br>-Utoaji wa elimu ya uhifadhi wa mazingira<br><br>-Kuelimisha na kuimarisha Kamati za mazingira za vijiji<br><br>-Kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali<br><br>-Mpango wa utekelezaji wa usimamizi wa misitu wa wilaya. | - Vitendea kazi duni (uvuvi)<br><br>-Ucheleweshaji wa fedha za retention (misitu)<br><br>-Kutoelimika kwa jamii<br><br>-Kutoeleweka kwa mipaka ya utawala.<br><br>-Uhaba wa watumishi<br><br>-Mawasiliano duni na wilaya jirani.<br><br>-Kuwepo barabara zisizo rasmi.<br><br>-Bajeti finyu. | - Kuanzisha mfumo wa mawasiliano na wilaya jirani (mtandao wa mawasiliano).<br><br>-Kuandaa mfumo wa uwiano wa ushuru na wilaya jirani.<br><br>-Kuboresha ushirikianokatika ngazi zote.<br><br>-Kufunga uvunaji wa magogo katika maeneo yaliyoharibiwa.<br><br>-Kuandaa na kutekeleza mpango endelevu wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya misitu ya Hifadhi ya Vijiji/binafsi.<br><br>-Uandaaji na utekelezaji mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi ya Taifa/Halmashauri. |
| MAFIA:<br>-Kamba<br>-Boriti<br>-Mkaa<br>-Samaki | -Kibanju<br><br>-Delta ya mto Rufiji<br><br>-Bandari kubwa na Ndogo | -Elimu ya mazingira<br><br>-Kuendesha doria.<br><br>-Kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali.<br><br>-Kushirikisha wanavijiji kubuni njia mbadala za kiuchumi.<br><br>-Kubadilishana mitego kwa kuchukua ile haribifu na kuwapa wavuvi mitego endelevu. | -Uvunaji wa matumbawe.<br><br>-Msongamano wa wavuvi kutoka nje ya wilaya.<br><br>-Viwanda vya kusindika samaki kuchagua mazingira. | -Utafiti wa athari za meli za uvuvi.<br><br>-Uimarishaji wa mawasiliano kati ya wilaya na wilaya.<br><br>-Kuandaa mpango wa kutembeleana kuona nini kinachofanyika katika wilaya ya Mafia. |

| **Aina ya Maliasili inayovuja/ Inayotoroshwa** | **Maeneo Husika** | **Hatua za kudhibiti** | **Matatizo yanayojitokeza** | **Njia za kusaidiana kudhibiti** |
|---|---|---|---|---|
| MKURANGA:<br>-Mbao<br>-Boriti<br>-W/pori<br>-Mkaa<br>-Magogo<br>-Samaki | Mjimwema hadi Kigamboni Dar.<br>Kibudi/ Bomu (Msangani ya FR) hadi Gongo la Mboto.<br>Kisarawe Malenda hadi Jaribu mpakani (Rufiji).<br>Dendeni FR hadi Zanzibar/ Dar es Salaam. | -Wizara, wiaya na jamii kuweka mipango ya matumizi endelevu ya maliasili.<br>-Kushirikisha jamii katika kuhifadhi maliasili.<br><br>-Kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa kazi. | -Mipaka ya kiutawala haieleweki.<br>-Ukosefu wa fedha za kutosha.<br><br>-Mwingiliano wa kiidara na kiwizara. | -Kupeana taarifa katika utekelezaji wa kazi.<br><br>-Jamii zipate manufaa kutokana na maliasili zinazowa-<br>Zunguka.<br>-Doria za pamoja.<br>-Kutoa motisha kwa mtoa taarifa .<br>-Mashindano ya shughuli za udhibiti kati ya wilaya na wilaya. |
| KISARAWE:<br>Mazao misitu<br><br>Mazao wanyamapori | -Vikumburu hadi Mloka (Rufiji) .<br>-Vikumburu hadi Morogoro.<br>-Vikumburu hadi Kibaha hadi Dar es salaam. | -Ushirikiano na taasisi za idara husika mfano, kikosi cha kuzuia ujangili.<br>-Kuweka vizuia.<br>-Kushirikiana na Asasi mbalimbali.<br>-Ushirikishwaji wa jamii.<br>-Kuchukua hatua za kisheria.<br>-Kutunga sheria ndogondogo za vijiji. | -Sheria zilizopitwa na wakati.<br><br>-Kucheleweshwa kwa kesi za maliasili. | -Kufanya mikutano ya pamoja.<br><br>-Kushirikisha vijiji vya mpakani katika ulinzi. |

# 2 Sehemu Ya Pili

**Maandalizi na kazi za vikundi**

## 2.1 Mgawanyo wa wanawarsha kwenye vikundi

Wanawarsha waligawanywa katika vikundi vitano kulingana na fani na uzoefu wao. Vikundi hivyo ni pamoja na (i) Misitu (ii) Uvuvi (iii) Wanyapori (iv) Utafiti, Taarifa na mawasiliano (v) Mipaka

Mwezeshaji wa kila kikundi alikuwa mtumishi wa wilaya ya Rufiji katika sekta husika.

## 2.2 Kazi za vikundi

Kila kikundi kilitakiwa kutaja matazizo yanayokabili sekta husika na kupendekeza njia za ufumbuzi

## 2.3 Mawasilisho ya vikundi

Mawasilisho ya matatizo na mapendekezo ya ufumbuzi yaliyotolewa na vikundi mbalimbali ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

**Jedwali Na. 2: Mawasilisho ya matatizo na mapendekezo ya ufumbuzi.**

**A) KIKUNDI CHA UVUVI**

| MATATIZO | MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI/UTATUZI |
|---|---|
| 1. Uvuvi wa meli na kokoro (Trawling) unaosabisha kuvuliwa kwa samaki wadogo wasiotumika ambao ni kizazi cha baadaye. | Kuwe na usimamizi thabiti wa mipaka kati ya eneo linaovuliwa na wenye meli na wavuvi wadogo.<br><br>Muda wa kuvua kwa meli upunguzwe yaani zipewe leseni za miezi sita badala ya miezi tisa.<br><br>Waangalizi katika meli wawe wa kutoka katika wilaya husika na sio kutoka wizarani tu.<br><br>Nyavu za meli ziwe na macho zaidi ya inchi mbili ili kumaliza tatizo la kumwaga dagaa.<br><br>Idadi ya meli ipunguzwe na kuwa meli nne kwa zoni.<br><br>Kila sehemu kuwe na utaratibu wa kubadilishana mitego kutoka mitego haribifu na kutoa mitego endelevu. |
| 2. Msongamano wa wavuvi kutoa nje ya wilaya husika | Sheria ndogo zitungwe ili kudhibiti idadi ya wavuvi wahamiaji yaani kila kijiji kipokee idadi maalum ya wavuvi. Hii ifanyike baada ya utafiti. |
| 3. Uvunaji wa matumbawe | Sheria zipo ila usimamizi wake ni hafifu. Kwa hiyo serikali za vijiji husika zishirikishwe pamoja na kamati za mazingira kusimamia suala hili.<br><br>Kupitia wataalam wananchi wapewe maelekezo ya kutumia vifaa vingine vya ujenzi badala ya kuchoma matumbawe. |
| 4. Tatizo la mmomonyoko wa fukwe | Wenye mashua wasichukue mchanga wa farruum au peto kwenye ufukwe wa bandari badala yake wakachukue kwenye mafungu au baharini. |
| 5. Utoroshaji wa samaki na kamba nje ya wilaya | Udhibiti wa ushuru usimamiwe na vijiji husika na utaratibu wa utoaji wa asiimia kwa wahusika urekebishwe ili kuondoa urasimu.<br><br>Halmashauri husika ibinafsishe ukusanyaji wa ushuru. |

## (B) KIKUNDI CHA MIPAKA

| **KIKUNDI CHA MIPAKA** | |
|---|---|
| **MATATIZO** | **MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI/UTATUZI** |
| 1. Kutokueleweka kwa mipaka kati ya wilaya na wilaya-Mkuranga na Rufiji<br>-Kisarawe na Rufiji<br>-Kisarawe na Mkuranga<br>Kutokana na kutokuwepo kwa alama maalum katika maeneo ya mpakani jambo linalosababisha mgongano hususan wakati wa ukusanyaji mapato ya Halmashauri na vijiji yatokanayo na mazao ya maliasili.<br>2. Uanzishwaji vijiji bila kujali/kuweka mipaka | Kukamilisha makubaliano kwa kuweka alama kwenye maeneo yenye utata mipakani mwa wilaya husika.<br><br>Kuandaa mkakati wa kutembelea maeneo yenye utata kwa kushirikisha wataalamu, uongozi wa vijiji na wilaya<br><br>(iii) Sheria ya ardhi ya vijiji Na. 5/1999 izingatiwe katika kuanzisha na kusimamia vijiji kuwa na mipaka. |
| **KIKUNDI CHA WANYAPORI** | |
| 1. Ujangiri | Wananchi washirikishwe kikamilifu kwenye shughuli za uhifadhi<br>Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kufanya doria za pamoja kati ya mradi wa Selous na wilaya za Mkuranga (Rufiji/Kisarawe)<br>Vizuia vya ukaguzi wa mazao ya maliasili viimarishwe na kuboreshwa<br>Kuimarisha na kuboresha vitendea kazi<br>Kuwa na mawasiliano imara kati ya Mradi wa Selous na wilaya za Kisarawe, Mkuranga na Rufiji. |
| 2. Uwindaji usiozingatia wanyama waliokatiwa leseni/maeneo ya uwindaji | Kuimarisha usimamizi wa sheria ya uwindaji<br>Kuelimisha wawindaji juu ya taratibu za maeneo ya uwindaji<br>Kuimarisha ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya uwindaji<br>Mipaka ya wilaya ieleweke |
| 3. Wanyama waharibifu | Halmashauri za wilaya na vijiji kutenga fedha za kununulia nyavu na risasi za aina mbalimbali.<br>Vijiji viandae na kutekeleza mpango endelevu wa matumizi bora ya ardhi. |
| 4. Uhaba wa watumishi | Halmashauri ziombe vibali vya kuajili<br>Wanavijiji wawezeshwe kufanya baadhi ya shughuli za uhifadhi |
| 5. Ujenzi holela wa hoteli za kambi za uwindaji | Wilaya zihakikishe kuwa wawekezaji wana leseni hai<br>Wilaya ziwe na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi<br>Wilaya zitunge sheria ndogo kuhusiana na matumizi ya ardhi |
| 6. Kesi za nyara/maliasili kuchukua muda mrefu | Kuimarisha uhusiano mzuri na vyombo vyote vya dola<br>Kuimarisha Elimu kwa wananchi<br>Wahalifu wa makosa madogo walipefaini baada ya kukiri makosa. |

### (C) KIKUNDI CHA MAWASILIANO TAKWIMU NA UTAFITI

| MATATIZO | MAPENDEKEZOYA UFUMBUZI/UTATUZI |
|---|---|
| Mawasiliano:<br>Vyombo vya mawasiliano k.m. radio/simu<br><br><br><br><br><br><br><br>Taarifa za kazi | 1. Pale inapowezekana msaada wa simu za upepo za radio za Polisi (radio call) zitumike<br>Masafa ya simu za upepo (radiocalls) zilizopo kwenye vituo mbalimbali vya aliasili yarekebishwe (Harmonization of radio frequencies) ili kuwezesha mawasiliano na pia kuanzisha vituo vipya kwa maeneo yasiyo na radio.<br>Kuangalia uwezekano wa kila wilaya kuwa na tarakilishi itakayowezesha kuunganishwa kwenye mtandao wa matumizi ya barua pepe (e-mail).<br>(i) Kuwa na utaratibu wa kupeana nakala za taarifa za kazi kwa vipindi vya robo/nusu mwaka na mwaka.<br>Kuanzisha kijarida cha pamoja kitakachotolewa mara mbili kwa mwaka. |
| 2. Takwimu | Wilaya ziwezeshwe kukusanya takwimu<br>Utaratibu uandaliwe (wa lazima) utakaowezsha wilaya kupata takwimu zilizokusanywa na wadau mbalimbali.<br>Takwimu za aliasili za wilaya ziwe wazi kwa wilaya nyingine.<br>Mfumo wa utunzaji takwimu kwenye tarakilishi (computer) uainishwe. |
| 3. Utafiti | Taarifa za matokeo ya utfiti unaofanywa na wadau mbalimbali zipelekwe katika wilaya husika na nakala kwa wilaya jirani pamoja na wadau wengine stahili.<br>Utafiti wa raslimali katika wilaya uhusishe wilaya jirani. |

### (D) KIKUNDI CHA MISITU

| MATATIZO | MAPENDEKEZO YA UFUMBUZI |
|---|---|
| 1. Utoroshaji wa mazao ya misitu bila kulipia | Wasimamizi wa sheria wawe makini sana. |
| 2.Kutumia vibali zaidi ya mara moja | Kuimarisha vizuia na kufanya doria mara kwa mara. |
| 3. Matumizi mabaya ya hati za kusafirishia | Kuthibiti njia au mianya ya utoroshaji. |
| 4. Kugushi leseni | Wasimamizi wa sheria wawe makini katika wilaya na vizuia vyote. |
| 5. Udhaifu katika vizuia:-<br>-Elimu ndogo<br>-Uaminifu mdogo<br>-Fani tofauti<br>-Upungufu wa watumishi | -Watumishi waliopo wapewe elimu<br>-Kuajiri watumishi wenye fani husika.<br>-Kuchukua hatua za kinidhamu stahili kwa watumishi wanaokiuka maadili. |
| 6. Matumizi mabaya ya vizuia | Vizuia vitumike kukagua mazao ya msitu na sio kutoa leseni za uvunaji mazao ya misitu |
| 7.Mioto nyakati za kiangazi | Wananchi waelimishwe kutumia sheria ndogo za kudhibiti moto. |
| 8. Mwingiliano wa kisekta | Mikutano ya kutafuta muafaka wa maingiliano ya kisekta ifanyike na kuandaa mkataba wa makubaliano |
| 9. Kiwango cha chini katika ushirikishwaji | Juhudi ziongezwe za kuwaelimisha na kuwapa nguvu wananchi kushiriki katika usimamizi wa misitu/maliasili. |
| 10. Mapungufu katika sheria | Sheria kuu haitaji wazi kiwango cha faini kwa kosa lililotendeka. Kwa mfano usafirishaji wa mazao ya misitu usiku faini isizidi sh. 300,000/=. Hivyo sheria ifanyiwe marekebishao |
| 11. Vitendea kazi | Vitendeakazi viongezwe na pale ambapo havipo vitolewe |

## 2.4 Kazi ya pili ya vikundi

### 2.4.1 Baada ya mawasilisho ya awali

Baada ya mawasilisho ya awali, wanawarsha walirudi tena kwenye vikundi vyao kuchagua mkakati wa kupewa kipaumbele kati ya yale yaliyorodheshwa kwenye sehemu ya "mapendekezo ya ufumbuzi/utatuzi". Aidha walitakiwa kuonyesha atakayehusika na utelekezaji wa mkakati huo, kwenye eneo lipi kuanzia lini, kwa muda gani na kwa gharama ipi (Bajeti).

Kabla ya kufanya kazi hii, wanawarsha walitaka kujua kama kuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya mikakati itakayochaguliwa ambapo walijibiwa na mwezeshaji kuwa ni vizuri ikaandaliwa bajeti ambayo inaweza kuombewa fedha kwa serikali au wahisani, vinginevyo ni vigumu kuomba fedha bila kuwa na mpango wa utekelezaji unaoambatana na bajeti.

### 2.4.2 Baada ya kazi kwenye vikundi mawasilisho yalikuwa kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 3: Mawasilisho Ya Vikundi**

| SHUGHULI | MHUSIKA | WAPI | LINI | MUDA | BAJETI (SH.) |
|---|---|---|---|---|---|
| UVUVI: Kuimarisha usimamizi wa ushuru wa kamba na samaki wanaotoka nje ya wilaya. | Halmashauri, serikali za vijiji, kamati za mazingira na ofisi za vitongoji | Kijiji na kwenye vizuia | Januari 2004 | Miezi mitatu | 2,240,000/- |
| MIPAKA: Kutembelea vijiji vyote mpakani vyenye mgogoro | Maafisa Ardhi, Halmashauri, Wanavijiji | Rufiji, Mkuranga na Kisarawe | Jan. 2003 | Miezi miwili | 1,640,000 |
| Kuandaa mikutano na viongozi pamoja | -do | -do- | Jan. 2003 | | |
| Kuweka alama rahisi zinazoonyesha mipaka ya wilaya | -do- | Wilaya husika | Jan. 2003 | Miezi mitatu | 3.050,000/= |
| Kupeleka viongozi kwenye maeneo husika | -do- | Wilaya husika | Jan 2003 | Miezi mitatu | 3,585,000/= |
| **JUMLA** | | | | | **8,275,000** |
| MISITU: Usimamizi shirikishi misitu | DFO, DALDO, DGO, CDO, Wafadhili na wanakijiji. | Mtita, Masanganya, Pombwe, Ruvu kusini, Mloka, Vikumburu, Mchungu | Jan. 2003 | Miaka mitatu | 60 milioni |
| Doria za pamoja | DFOs na Vyombo vya usalama. | Maeneo ya wilaya husika | Jan.-Des. 2003 | Siku 60 kwa mwaka | 15 milioni |
| MAWASILIANO<br>-Kununua radio call 2 kwa wilaya ya Mkuranga na Mafia.<br>-Kuoanisha mawimbi ya radio kwa wilaya jirani. | DED/DNRO | Mafia/ Mkuranga Rufiji, Mafia, Mkuranga, kisarawe na Kilwa. | 2004<br><br>2003 | Miezi 6<br><br>Miezi 6 | 10 milioni<br><br>1 milioni |
| Kuweka mtandao wa simu pepe kwa kutumia simu za kawaida | DED/DNRO | Mafia, Mkuranga, Kisarawe | 2004 | Miezi 3 | 3 milioni |
| WANYAMAPORI:<br>Uzuiaji ujangili | DGOs na Askari wa vijiji | Mapori nje ya Selous | 2003 | Zoezi la kudumu | 1,102,000/= |
| Ununuzi wa risasi | DED/DGO | Mzinga, AISCO na WD | Jan. 2004 | | 4,460,000/= |
| Ununuzi wa nyavu | DED | Kiwanda cha nyavu | Jan. 2004 | | Nyavu 10 @ wilaya 300,000/= = 3,000,000/ |

# 3 Sehemu Ya Tatu

## 3.1 Muhtasari wa mada mbalimbali zilizowasilishwa kwenye warsha

Baada ya kupitia mada zilizotolewa, mambo yaliyojitokeza kwenye majadiliano ya wanawarsha ni pamoja na:

### 3.1.1 Hali halisi ya maliasili, usimamizi na matumizi

- Wilaya zetu kuwa na utajiri wa maliasili mbalimbali ikiwa ni pamoja na misitu, bahari na mazao ya uvuvi ambayo ni pamoja na Kamba fukwe, Nyuki, na maeneo ya mambo ya kale.
- Sehemu kubwa ya malisili hizi zimekuwa zikitegemewa na serikali kuu pamoja na serikali za Halmashauri ya wilaya kama vyanzo vikuu vya mapato.
- Utegemezi huu mkubwa umekuwa chanzo cha uvunaji usiozingatia uwiano kati ya mavuno na hali halisi ya maliasili husika, jambo ambalo linahatarisha kuwepo kwa maliasili hizo na kusabisha uharibifu wa mazingira.
- Pamoja na uvunaji huo Halmashauri za wilaya zimekuwa haizifaidiki sana kutokana na sehemu kubwa kupelekwa serikali kuu na kutoroshwa kupitia njia zisizo rasmi.

Katika kulinda na kutumia maliasili hizo njia mbalimbali zimekuwa zikitumiwa ikiwa ni pamoja na:

- Doria za mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti uhalifu;
- Ushirikishaji wananchi kwa njia mbalimbali katika ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu;
- Matumizi ya vizuia kwa lengo la ukaguzi ili kudhibiti uhalifu;
- Utoaji leseni kwa lengo la kudhibiti viwango vya uvunaji,
- Utoaji elimu juu ya uhifadhi kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mikutano, semina, warsha, kongamano, vipeperushi, vijarida, vipindi vya radio, luninga, n.k;
- Kamati mbalimbali za uhifadhi wa mazingira zimeendelea kuundwa na kutumiwa katika ngazi mbalimblai za wilaya;
- Utungaji wa sheria ndogo kwa lengo la kulinda mazingira; na
- Kushirikiana na Taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa umechangia katika suala zima la uhifadhi.

### 3.1.2 Matatizo ambayo yamejitokeza

- Usimamizi dhaifu wa maliasili kutokana na uhaba wa vitendea kazi, elimu ndogo kwa watumishi, motisha na bajeti finyu ya kutekeleza programu nzima ya uhifadhi wa maliasili.
- Mamlaka za halmashauri kuwa na lengo kubwa bila kujali uwezo wa maliasili husika.
- Mipaka isiyoeleweka ambayo imekuwa ikisababisha migogoro na uvunaji holela na kuzikosesha halmashauri husika mapato halali.
- Udhibiti mdogo wa mapato ya serikali kuu na halmashauri za wilaya
- Migongano kati ya wanyamapori na binadamu hasa kwa masuala ya wanyamapori kuhatarisha mali na maisha ya binadamu.

### 3.1.3 Mafanikio

Licha ya matizo mbalimbali

- Maliasili zingine zimeendelea kuwepo kutokana na juhudi za watumishi wachache waliopo wakisaidiana na taasisi mbalimbali.
- Mabadiliko katika sera na sheria za uhifadhi na matumizi ya maliasili na ardhi, ambazo zimelenga katika kumnufaisha mwananchi kwa kiasi kikubwa, zimebadili mtazamo wa wananchi kwa kuona maliasili kama sehemu ya maisha yao na si mali ya serikali tu kutokana na ushirikishwaji katika ulinzi na matumizi.

### 3.1.4 Mambo ya kufanya ili kuimarisha ulinzi na matumizi endelevu wa maliasili

- Kufanya doria za pamoja
- Kushirikisha wananchi wa vijiji vya mpakani katika shughuli za ulinzi.
- Kuandaa semina na warsha za pamoja (ujirani mwema) za mara kwa mara ili kufahamishana juu ya maendeleo ya mali asili na mabadiliko katika utendaji.
- Kujenga mfumo wa upeanaji wa taarifa kwa matukio yasiyo ya kawaida yanayohusu utoroshaji wa mazao ya maliasili kutoka wilaya moja hadi nyingine.
- Kuendelea kupanua wigo wa kushirikisha wananchi katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.
- Kushirikiana na mamlaka za wilaya katika kuangalia uwezekano wa kubinafsisha shughuli za ukusanyaji mapato ili wataalam waweze kufanya shughuli za ulinzi na udhibiti wa vitendo vya uhalifu kwa ufanisi.
- Mamlaka za halmashauri kujenga utamaduni wa kutoa kipaumbele kwa masuala ya utatuzi wa migogoro ya mipaka ili kuzuia maafa yanayoweza kujitokeza hapo baadaye.
- Ushirikiano kati ya serikali kuu na halmashauri katika kuangalia uwezekano wa kuajiri watumishi wenye elimu ya fani zinazotakiwa.
- Kuangalia uwezekano wa kufanya tafiti kwa kushirikiana na taasisi nyingine ili kujua viwango halisi vya uvunaji kwa kuzingatia ukubwa wa malisili zilizopo.
- Kuendelea kufanya tafiti na matumizi ya miradi mbadala ili kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa rasilimali za maliasili.

## 3.2 Tathmini ya warsha

**(Mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza katika warsha)**
Mbinu iliyotumika kufanya tathmini ilikuwa ya kumpa kila mwanawarsha kadi ya kuandika majibu ya maswali yafuatayo:-

- Umependa nini?
- Umetambua nini kilichokuwa na upungufu?
- Jambo gani ambalo ungeshauri libadilishwe/lifanyiwe marekebisho kama ingeandaliwa warsha nyingine?

Tathmini hii ilihusisha wanawarsha 25 wengi wao wakiwa wataalamu kutokana na wanawarsha viongozi (Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya) kuondoka mapema kwa sababu zisizozuilika. Maoni ya wanawarsha yamepangwa kwa kuzingatia mambo manne ambayo ni:-

1. Mahusiano kati ya mada zilizotolewa na lengo kuu la warsha.
2. Njia/mbinu (vikiwemo vifaa na mashine) zilizotumika kuhakikisha kuwa lengo la warsha linafikiwa.

3. Ushiriki wa wanawarsha.
4. Utawala na uendeshaji wa warsha pamoja na ukumbi.

Kwa ujumla washiriki walikiri kuwa mada kuu ya uvujaji (utoroshaji) wa maliasili nje ya wilaya ilikuwa sahihi na ilitoa fursa ya wilaya jirani kujifunza na kupanga mikakati ya pamoja. Walitoa shukurani kwa kupata fursa ya kubadilishana taarifa za utendaji, kujifunza na kupata uzoefu kutoka kwa wilaya nyingine. Pia walielezea matumaini yao ya uboreshaji wa mahusiano na ushirikiano baina ya watumishi wa wilaya husika. Aidha walipongeza ushiriki wa wataalamu wa masuala ya ardhi kwa kuwa changamoto kubwa katika utunzaji na uhifadhi wa maliasili.

Mafanikio mengine yaliyotajwa ni pamoja na ushiriki wa wanasiasa uliowawezesha kufahamu maoni ya wataalamu, mapokezi na maandalizi mazuri, utoaji wa nafasi sawa za kutoa mawazo kwa washiriki na fursa adimu ya watumishi kukutana, kufahamiana na kujadili matatizo ya kiutendaji. Pamoja na mafanikio, waliyataja mapungufu yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na muda mfupi wa warsha kukwama kufanya ziara ya kuutembelea msitu kutokana na hali mbaya ya hewa, kutoshiriki kwa wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za wilaya, uwiano wa kijinsia usio kuwa sawa na utunzaji wa muda kama ulivyoonyesha kwenye ratiba kutokana na viongozi wa kisiasa kuzungumzia jambo moja kwa muda mrefu. Muhtasari wa tathmini ya washiriki ni kama ulivyoonyeshwa hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Muhtasari: Tathmini Ya Washiriki na Warsha**

| **Suala** | **Walichopenda** | **Walichotambua kuwa na mapungufu** | **Walichoshauri kufanyika katika warsha nyingine** |
|---|---|---|---|
| 1. Mahusianao ya mada na lengo kuu la warsha | Fursa ya kujifunza kubadilishana habari<br>Mada kuu ya uvujaji wa maliasili ni sahihi<br>Ushiriki wa wanavijiji | Hakuna | Kuwa na warsha nyingine kufuatilia maazimio ya warsha. |
| 2. Njia/mbinu, vifaa mashine | Kufanya kazi kwenye vikundi<br>Fursa sawa ya kuongea<br>Kuheshimu mawazo ya kila mmoja | Kuahirishwa safari ya msituni<br>Utunzaji mbaya wa muda | Safari ya porini kuona wanyamapori.<br>Kutumia mashine za kisasa wakati wa kuwasilisha mada (overhead projector, Power Point).<br>Kuboresha utunzani wa muda.<br>Kutoa nakala za mada kwa kila mshiriki. |
| 3. Ushiriki | Mchanganyiko wa washirki kutoka kila wilaya.<br>Washiriki walikuwa wachangamfu.<br>Kukutana na marafiki wapya.<br>Kushirikiana mawazo na matatizo.<br>Mchanganyiko wa wanasiasa na wataalam. | Jinsia haikuwakilishwa ipasavyo. Wengi walikuwa wanaume.<br>Wadau wengine hawakushiriki.<br><br>Wanasiasa wote kutokuwepo siku ya pili. | Kuboresha mambo ya jinsia<br>Kutoruhusu wanasiasa kuumbua wataalam. |
| 4. Uendeshaji, Utawala na ukumbi | Ukarimu.<br>Mapokezi mazuri.<br>Chakula kizuri. | Choo kichafu, kiasi cha posho kidogo, muda mfupi wa warsha. | Barua za mwaliko zitumwe mapema kupata muda wa maandalizi.<br>Posho zaidi.<br>Muda zaidi.<br>Choo kizuri. |

## 3.3 Maazimio ya warsha

Baada ya mawasilisho na michango mbalimbali wanawarsha walitoa maazimio ya warsha kama ifuatavyo:

1. Suala la mipaka hasa utatuzi wa migogoro kati ya wilaya na wilaya, wilaya na hifadhi, lipewe kipaumbele badala ya kusubiri migogogo kutokea.
2. Mipango ya usimamizi bora ya ardhi na maliasili iandaliwe na Halmashauri za wilaya
3. Wananchi wawezeshwe na mamlaka zilizopo kusimamia vizuri maliasili zote zinazowazunguka.
4. Doria za pamoja kwenye maeneo ya uvunaji wa maliasili mipakani, ziandaliwe na kuimarishwa.
5. Utafiti ufanyike kujua hali halisi ya rasilimali iliyopo (samaki, kamba, misitu na wanyamapori) ili kuandaa vigezo halisi vya viwango vya uvunaji.
6. Utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa mapato ya serikali, halmashauri na vijiji kutokana na kamati uandaliwe kwa kushirikisha wadau wote na serikali kuu.
7. Utaratibu uandaliwe wa kuwezesha kiasi fulani cha fedha zilizokusanywa kutokana na mazao ya maliasili kibakie wilayani kuendeleza shughuli za uhifadhi.
8. Utafiti ufanyike kwenye eneo linalodhaniwa kuwa ni mazalia ya kamba kusini mwa Bwejuu (Kijiwe Nyara) hadi Kilwa kwa lengo la kulithibitisha ili lihifadhiwe.
9. Wafugaji wadogo wa samaki na kamba wahamasishwe na kuendelezwa na Halmashauri za wilaya
10. Warsha za pamoja (ujirani mwema) zifanyike angalau mara moja kwa mwaka.
11. Kila halmashauri iandae orodha ya rasilimali zilizopo kwenye wilaya yake kwa lengo la kuandaa mkakati wa uhifadhi wake

## 3.4 Kufunga Warsha

Wakati wa kufunga, Ndugu J. K. Bukwali mshauri wa maliasilili na mazingira katika sekretarieti ya mkoa wa Pwani ambaye alikuwa mwezeshaji wa warsha, aliombwa na kukubali kuwa mgeni rasmi.

Akifunga warsha hiyo, alishukuru ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji hususan Idara ya Ardhi Maliasili na Mazingira wilayani Rufiji kwa maandalizi mazuri ya warsha. Aidha aliwashukuru washiriki wote kwa michango yao ya mawazo ambayo iliweza kufanikisha malengo ya warsha.

Aliwaomba washiriki wote kushirikiana na mamlaka zao katika kutekeleza maazimio ambayo yamo ndani ya uwezo wa mamlaka hizo. Aliwashauri pia kuangalia uwezekano wa kutafuta wahisani kutoka ndani na nje kufadhili shughuli za utekelezaji wa maazimio ambayo mamlaka zao hazina uwezo nayo.

**Mkuu wa Mkoa, Mhs. N. Banduka anamtambulisha Mzee R. Koge, Mjumbe wa Kamati ya Mazingira, Kijiji cha Twasalie kwa warsha.**



Mwisho alishukuru uongozi wa mradi wa uhifadhi mazingira Rufiji (MUMARU) kwa kumwezesha kuendesha warsha iliyompa nafasi ya ziada ya kuboresha uelewa wake wa matatizo ya usimamizi wa mazingira kwenye ngazi za wilaya na vijiji.

Baada ya kusema hayo alitamka rasmi kufungwa kwa warsha.

# 4 Viambatisho

## 4.1 Kiambatisho Namba 1: Ratiba Ya Warsha

Halmashauri ya Wilaya Rufiji Warsha ya "Ujirani Mwema na Rufiji"

**Ratiba siku ya Kwanza (1)**

| **Muda** | **Tukio** | **Mhusika** |
|---|---|---|
| 2.00-3.00 | Kujiandikisha | Sekretariet |
| 2.30 | Makaribisho | Mkuu wa Wilaya, Rufiji |
| 2.40-2.45 | Madhumuni ya Warsha | Afisa Mshauri wa Masuala ya Maliasili na Mazingira Mkoa -(Mwezeshaji wa Warsha) |
| 2.45-3.00 | Ufunguzi rasmi wa warsha | Mkuu wa Mkoa, Pwani |
| **3.00** | **Chai** | **Wote** |
| 3.30 | Ziara ya Mafunzo kuhusu uvunaji holela wa misitu Rufiji | Wote |
| **7.00** | **Chakula** | **Wote** |
| 8.00 | Shughuli ambazo zimefanywa na wilaya ya Rufiji katika kusimamia mazingira | Afisa Ardhi Maliasili na Mazingira, Rufiji |
| 8.10 (Dakika 15 kwa ripoti) | Maelezo kutoka wilaya na taasisi yahusuyo aina, sehemu na kiasi cha uvunaji ("leakage") wa mazao ya maliasili (hasa mbao, mkaa, boriti, wanyamapori, mazao ya majini , hatua zinazochukuliwa kudhibiti, mafanikio, matatizo na maeneo ya ushirkiano ambayo yanaweza kusaidia katika kuboresha usimamizi wa maliasili. | 1. Wilaya ya Rufiji<br>2. Wilaya ya Mafia<br>3. MIMP<br>4. Wilaya ya Kisarawe<br>5. Hifadhi ya Selous na WWF<br>6.Wilaya ya Mkuranga<br>7.Wilaya ya Kilwa<br>8.Upotevu wa mazao ya kapa (kanda za Kati na Kusini). |
| **10.40** | **Chai** | **Wote** |
| 11.00 | | Mwezeshaji |
| | Jinsia na usimamizi wa Maliasili | Mwezeshaji wa Warsha |
| 2.00 | Video kama inapendwa | Sekretarieti |

**Siku ya Pili**


| **Muda** | **Tukio** | **Mhusika** |
|---|---|---|
| 2.00 | Kujiandikisha | Sekretarieti |
| 2.30 | Usimamizi wa Maliasili na mazingira na jamii-uzoefu wa wanavijiji wa Rufiji | Wawakilishi wa Kamati za mazingira kutoka vijiji vya Jaja, Twasalie, (Pwani/visiwani), na Mbunjumvuleni na Mtanzasona (bonde la Mto Rufiji |
| 3.00 | Maswali na Mazungumzo | Mwezeshaji wa muda – Mshauri wa maendeleo ya Jamii, MUMARU |
| 3.15 | Chai | Wote |
| 2.45 | Muhtasari wa taarifa na mawazo ya jana yahusuyo udhibiti wa uvunaji ("leakage") wa maliasili | Mwezeshaji |
| | Njia za kuelekea mbele kwa pamoja. Maandalizi ya vikundi | Mwezeshaji |
| 4.00-5.00 | Kazi ya vikundi | Wawezeshaji na wote |
| 5.00 | Mawasiliasho ya vikudi | Wawakilishi wa vikundi |
| 6.00 | Muhtasari na majadiliano | Mwezeshaji |
| **7.00** | **Chakula** | **Wote** |
| 8.30 | Mawasilisho ya vikundi | Wote |
| 9.30 | Muhtasari, majadiliano, maazimio, Mipango, **soda** | Mwezeshaji/Wote |
| 10.30 | Kufunga warsha rasmi | Mgeni Rasmi |

## 4.2 Kiambatisho Namba 2: Washiriki wa warsha

| Na. | Jina | Cheo | Unakotoka |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. N.M. Banduka | Mkuu wa Mkoa wa Pwani | Kibaha |
| 2. | Capt. James Yamungu | Mkuu wa Wilaya | Kisarawe |
| 3. | Ignas mashengere | Afisa Wanyamapori | Kisarawe |
| 4. | E.N. Mushi | Afisa Maliasili | Kisarawe |
| 5. | Rwegasira Leo | Afisa Ardhi Wilaya | Kisarawe |
| 6. | Pascal Kabeho | Afisa Wanyamapori Wilaya | Kisarawe |
| 7. | Brg. Gen. S. Hemed | Mkuu wa Wilaya | Rufiji |
| 8. | N. Kissenga | Afisa Nyuki Wilaya | Rufiji |
| 9. | A. Minde | Afisa Misitu Wilaya | Rufiji |
| 10. | M.S. Chande | Afisa Maliasili, Ardhi na Mazingira | Rufiji |
| 11. | E.B. Chirwa | Afisa Uvuvi wa Wilaya | Rufiji |
| 12. | M. Ngwalima | Afisa Mipango Wilaya | Rufiji |
| 13. | Z.M. Ngatanda | Afisa Ardhi Wilaya | Rufiji |
| 14. | Frank Sima | Afisa Mikoko | Rufiji |
| 15. | Mkwaya | Diwani | Rufiji |
| 16. | John Eniyoye | Afisa Wanyamapori Wilaya | Rufiji |
| 17. | Ramadhani Koge | Mwanakamati wa Maliasili/Kijiji | Twasalie |
| 18. | Amina A. Kiambwe | “ | Mbunju |
| 19. | Ismail Lusonzo | “ | Mtanzamsona |
| 20. | Athumani Aly | “ | Jaja |
| 21. | W.C. Malima | Afisa Mwakilishi WWF | DSM |
| 22. | L. Lukambuzi | Afisa Mwakilishi NEMC | DSM |
| 23. | Khanifa Karamagi | Mkuu wa Wilaya | Mkuranga |
| 24. | M. Kinana | Afisa Maliasili, Ardhi & Mazingira | Mkuranga |
| 25. | Michael Mmbongwa | Afisa Wanyamapori | Mkuranga |
| 26. | Suwedi Juma | Afisa Uvuvi | Mkuranga |
| 27. | Alphonce tiba | Afisa Ardhi | Mkuranga |
| 28. | A.Shola | Afisa Misitu | Mkuranga |
| 29. | Hassan Bendeyeko | Afisa Ardhi | Kibaha* |
| 30. | J. Bukwali | Afisa Maliasili Mshauri wa Mkoa | Kibaha |
| 31. | A.M. Libaba | Mkuu wa Wilaya | Mafia |
| 32. | M. Gwakirayi | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | Mafia* |
| 33. | I. Mtani | Afisa Uvuvi | Mafia |
| 34. | G.S. A. Melele | Mhifadhi –Hifadhi ya Bahari | Mafia |
| 35. | LT. W.F. Ligibu | Mkuu wa Wilaya | Kilwa* |
| 36. | M. Senyagwa | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | Kilwa* |
| 37. | S. Mizabwa | Afisa Maliasili Wilaya | Kilwa* |
| 38. | M. Mfangavo | Afisa Misitu Wilaya | Kilwa* |
| 39. | Ismail Kilobo | Diwani | Chumbi |
| 40. | R. Mongogwela | Msaidizi wa Mkuu wa Mkoa | Kibaha |
| 41. | Jonas Nambua | Afisa Misitu | Utete |
| 42. | Esther Mshana | Mwakilishi wa Radio Tanzania | Kibaha |
| 43. | Selina Wilson | Mwakilishi Uhuru/Mzalendo | Kibaha |
| 44. | A. Budondi | Mpiga picha TVT | DSM |
| 45. | G. Pondamali | Afisa Usalama | Utete/Rufiji |

N.B: * Hawakuhudhuria warsha

**Mdg. M.S. Chande , Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira , Wilaya ya Rufiji**







## 4.3 Kiambatisho Namba. 3: Hotuba ya Mgeni Rasmi

Hotuba iliyotolewa na Mgeni Rasmi, Mheshimiwa N.M. Banduka, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, katika warsha ya "Ujirani Mwema na Rufiji" iliyofanyika Ikwiriri tarehe 3-4 Desemba, 2002

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Waheshimiwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira, Wakuu wa Taasisi mbalimbali, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Nakuchukua fursa hii kuwashukuru kwa kukubali wito wa kufika kwenye warsha hii, hivyo kuwa tayari kuchangia katika mada mbalimbali ambazo zitasaidia kuboresha usimamizi wa maliasili na mazingira wilayani Rufiji na pia katika wilaya zenu.

Pia nachukua fursa hii kuishukuru wilaya ya Rufiji kwa kuona umuhimu wa kuandaa warsha hii.

Maliasili katika wilaya zetu kwa kiasi kikubwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa wilaya zetu. Kwa mfano, takwimu zilizopo wilayani Rufiji zinaonyesha kuwa asilimia 75 ya mapato yake yanatokana na maliasili. Hata hivyo mchango wa maliasili hizo hauthaminiwi kutokana na usimamizi duni. Maliasili hizo zingeweza kuwa na manufaa zaidi kama zingesimamiwa vizuri. Hivyo kuongeza pato la wilaya na kuinua uchumi wa wananchi kwa ujumla.

Sababu kubwa zinazosababisha usimamizi duni wa maliasili zinaweza kugawanywa katika makundi mawili.

- Kundi la kwanza ni sababu za kiuchumi
- Kundi la pili ni sababu za kiutawala

<u>**Sababu za Kiuchumi**</u>

**Uthamini usio sahihi**
Mara nyingi watendeji ambao ndio wenye uamuzi wana tabia ya kupima zao au tumizi moja tu la maliasili fulani. Kwa mfano katika maliasili ya msitu wanathamini mbao peke yake bila kujali uhusiano wa mti huo na viumbe wengine ikiwa ni pamoja na nyuki, ndege, wanyamapori, uwezo wa msitu kuzalisha hewa safi na uhusiano wake na hifadhi ya ardhi. Pia wanasahau kupima thamani ya kuni, madawa, matunda, mazao nyuki, wanyamapori na wadudu wanaoweza kuwa na thamani ya kufugwa au kwa shughuli za kitalii. Kwa hali hiyo ukataji wa msitu kwa ajili ya mbao unainyima wilaya nafasi nyingine nyingi za kiuchumi. Kwa misingi hiyo ipo haja ya kuangalia maliasili kwa mtazamo mpana ili kuwa na uwiano wa matumizi endelevu.

**Mapato ya haraka yanayosababisha uharibifu**
Sababu nyingine ya kiuchumi ni kwamba faida kubwa itokanayo na matumizi yasiyoendelevu inafanywa na matajiri amao hawajali maisha ya baadaye ya watu kwa maeneo husika. Wanaochoeleza ni kuwa ni bora wakamaliza maliasili hizo kwa sababu hawatakuwepo kesho. Kwani watatafuta sehemu nyingine za uvunaji . Utaratibu huo umesababisha miti kama Mininga, Mvule na Mpingo kuwa katika hatari ya kutoweka, kwani hata miti midogo inavunwa. Hatari hii ipo pia katika uvunaji wa kamba ambapo mazalia ya amaki yanaharibiwa na vyombo vikubwa vya uvuvi.

Hata wenyeji wengine wameingia kwenye mkumbo wa uharibifu kwa kutafuta faida ya haraka bila kujali athari za muda mrefu. Hii imesababishwa na umaskini na kutokuwa na shughuli mbadala. Aidha sababu nyingine ni mawazo finyu kuwa maliasili hizo zitakuwepo milele, hivyo haziwezi kwisha. Kasumba iliyopo ni kuwa "kama sitachukuwa mimi, mwingine atachukua. Hivyo kwa nini nisichukue?".

Wavunaji wadogo na wakubwa hawana motisha wa kuwafanya wavune mazao kwa viwango endelevu. Faida kubwa kwa muda mfupi ndio mwelekeo wa wote.

## Sababu za kiutawala

### Uwezo mdogo wa Halmashauri

Kutokana na vyanzo vichache vya mapato kuendesha shughuli za Halmashauri, Halmashauri zimejikuta zikiegemea kwenye maliasili kama njia rahisi ya kukusanya mapato bila kujali uwezo wa maliasili hizo kuhimili uvunaji. Aidha uhaba wa watumishi umechangia katika usimamizi duni wa maliasili. Baadhi ya wakusanyaji ushuru sio wataalamu wa maliasili. Hivyo hawana elimu ihusianayo na athari za uvunaji wa baadhi ya aina za maliasili na mahali zitokako. Pamoja na mapato makubwa ni sehemu ndogo inayorudishwa kwenye shughuli za hifadhi. Jambo hilo linafanya sehemu kubwa ya mazao kuibiwa, kutokana na uhaba wa doria na udhibiti, hivyo kukosesha halmashauri mapato halisi. Sababu nyingine za kiutawala ni mkanganyiko wa nani ana simamia nini kutokana na kuchelewa kupitishwa kwa sheria za usimamizi wa maliasili licha ya kuwepo kwa sera zinazowapa wananchi uwezo wa kusimamia maliasili hizo.

Kutokana na matatizo haya inakisiwa kwamba ni asilimia 10 tu ya mapato yanayokusanywa kutokanana na mazao ya maliasili wakati asilimia 90 inaibiwa, hivyo kusababisha hasara kubwa kwa halmashauri na wananchi kwa ujumla. Kwa hali hiyo wilaya zipo kwenye hali ya utajiri wa maliasili wakati halmashauri na wananchi wote wako kwenye hali ya umaskini.


Licha ya matatizo haya baadhi ya wilaya zimechukua hatua za kubadilisha hali hii, Rufiji ikiwa ni mojawapo. Kwa kipindi cha miaka minne mradi wa usimamizi wa mazingira kwa kushirikiana na halmashauri ya wilaya imebadilisha mtazamo. Wamefanya utafiti na kufahamu kiasi cha uharibifu na upotevu wa mazao ya maliasili ikiwa ni pamoja na misitu, wanyamapori na mazingira kwa ujumla. Wamejenga mwamko wa wadau wa ngazi zote kuthamini na kujadili matumizi endelevu ya malisili na mazingira. Aidha wamejenga uwezo wa wahusika kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya kutengeneza mipango ya uhifadhi na matumizi endelevu na utekelezaji wake.

Hata hivyo, wilaya moja peke yake haiwezi kudhibiti udhaifu ambao tumeuongelea hapo juu. Ni kwa kuzingatia hali hiyo wilaya ya Rufiji imeona umuhimu wa kuwaita majirani zake ili kubadilishana uzoefu, kufahamiana vizuri zaidi na kujenga mawasiliano mazuri, ili kujenga mkakati wa pamoja wa kusimamia vizuri maliasili.

Ni mategemeo yangu kuwa warsha hii itatoa maazimio madhubuti yatakayosaidia katika usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili katika wilaya zetu zote.

Baada ya kusema hayo natamka kuwa warsha hii imefunguliwa rasmi. Nawatakia kila la heri katika majadiliano.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mhs. Capt.James Yamungu na Mshauri wa Maliasili na Mazingira wa Mkoa Ndg. J. Bukwali



## 4.4 Kiambatisho Namba. 4: Sekta Ya Uvuvi Wilaya Ya Rufiji

### 4.4.1 UFAHAMU WA MALIASILI UVUVI ZILIZOPO WILAYA YA RUFIJI:-

Mto Rufiji
Stieglers Gorge
Mabwawa zaidi ya 13 ndani ya tambarare ya mafuriko, Ziwa Mtanza, Zumbi, Ruwe, Uba, Weme, Umwe, Ilu, Lugongwe n.k
Delta ya Rufiji
Bahari na mwambao wake

**SHUGHULI KUU** ni Kilimo na Uvuvi

**MAZAO YA MAJINI**
M.t 3,500 zenye thamani ya dola 800,000 kwa mwaka kutokana na kamba, (Prawns) wanaosafirishwa
Mbarata (Hilsa Kelee) wanao safirishwa nje ya wilaya
Uvuvi mdogo wa kamba mt. 2,200 kwa mwaka wenye dhamani ya dola 4 million
Uvuvi wa meli 80% ya kamba wote wanaovuliwa nchini Tanzania hutoka Rufiji delta

### 4.4.2 MATUMIZI HARIBIFU YA MALIASILI ZA UVUVI.

2.1. Uchafuzi wa mazingira ya bahari (Kiwanda cha TANPESCA)

- Takataka za mabaki ya samaki
- Madawa
- Kumwagika kwa mafuta
- Uchafu mwingine kutoka kwa binadamu

Madhara yanayotarajiwa:


- Kuharibika kwa ubora wa kamba
- Kupungua kwa wingi wa kamba
- Hatari kwa afya ya binadamu
- Kuharibu ubora wa hifadhi ya bahari wilaya jirani

**Ushauri:**
Utafiti wa kina ufanyike.
2.2. Uvuvi wa kamba wa kutumia meli (trawling- Industrial fishing)

| SN | Mwaka | Uvunaji Mt | Siku za kuvua | C.P.U.E |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 1988 | 550 | 7476 | 441 |
| 2 | 1989 | 688 | 2166 | 318 |
| 3 | 1990 | 960 | 1574 | 610 |
| 4 | 1991 | 670 | 1315 | 508 |
| 5 | 1992 | 663 | 1560 | 425 |
| 6 | 1993 | 590 | 1462 | 408 |
| 7 | 1994 | 1014 | 2513 | 403 |
| 8 | 1995 | 312 | 2108 | 385 |
| 9 | 1996 | 769 | 1779 | 432 |
| 10 | 1997 | 700 | 2091 | 334 |
| 11 | 1998 | 995 | 2778 | 358 |
| 12 | 1999 | 688 | 2252 | 505 |
| 13 | 2000 | 909 | 3352 | 271 |
| 14 | 2001 | 1193 | 3882 | 307 |

## WASTANI WA MAPATO KWA SIKU

| SN | Mwaka | Wastani Wa pamato kwa siku |
|---|---|---|
| 1 | 1988 | 500 |
| 2 | 1989 | 350 |
| 3 | 1990 | 600 |
| 4 | 1991 | 500 |
| 5 | 1992 | 480 |
| 6 | 1993 | 450 |
| 7 | 1994 | 400 |
| 8 | 1995 | 350 |
| 9 | 1996 | 400 |
| 10 | 1997 | 380 |
| 11 | 1998 | 400 |
| 12 | 1999 | 380 |
| 13 | 2000 | 350 |
| 14 | 2001 | 400 |




Baadhi ya wakazi wa vijiji vya uvuvi wa kamba wanaulalamikia uvuvi huo. Wanatambua kuwa hiyo ndiyo sababu ya uvuvi uliyokithiri kwenye mwambao wao. Meli (Trawlers) zinaendelea kuchimbua sakafu karibu na fukwe za bahari.

### 4.4.3 USHAURI

- Halmashauri zinazohusika kwa kushauriana na idara zifanye utafiti wa madhara ya uvuvi huu mapema
- Idadi ya lesseni ipunguzwe. Hivi sasa vipo zaidi ya meli 20.
- Muda wa msimu wa uvuvi ufupishwe

**Maswali yenye utata yanayokwamisha juhudi za wilaya katika kuhifadhi na kulinda maliasili**

- Uvujaji wa mapato ya halmashauri nje ya wilaya
- Kilo za kamba wanaokusanywa na wafanya biashara na viwanda hasa TANPESCA hazihakikiwi vizuri. Hivyo ushuru huvuja

**USHAURI**
Pawepo na msimamizi kwenye kiwanda.

**Tofauti ya thamani za ushuru wa raslimali baina ya halmashauri jirani. Wafanyabiashara hupata mpenyo wa kukwepa ushuru sahihi.**

**Ushauri.**
Ni muhimu kufahamu kuwa mapato yanayopatikana kutokana na maliasili zitumike katika kulinda raslimali hizo.

**Ufinyu wa fedha na nyenzo zinazoelekezwa kwenye usimamizi endelevu kuhusu elimu n.k**

## 4.5 Kiambatisho Namba 5: Uvunaji Wa Mazao Ya Misitu Kutoka Wilaya Ya Rufiji Na Kusafirishwa Wilaya Jirani

### 4.5.1 HALI HALISI

Hali halisi ya uvunaji wa mazao ya misitu kutoka wilaya ya Rufiji na kusafirishwa wilaya jirani ni mkubwa na wa muda mrefu.

Mazao ambayo yanavunwa na kusafirishwa nje ya wilaya kwenda jirani ni:-
1. Magogo ya aina mbali mbali
2. Mbao, mkaa na kongowele

Misitu inayovunwa mazao haya ni maeneo yote ya misitu ya hifadhi na ile ya wazi na inayopakana na bahari pamoja na wilaya jirani. Baadhi ya misitu hiyo ni:-

1. MTITA F/R
2. MCHUNGU F/R
3. KIKALE F/R
4. MTANZA MSONA F/R
5. RUHOI F/R

Na maeneo ya misitu isiyohifadhiwa ya makima, ugenzi, bundi n.k.

Aidha wavunaji hawafuati utaratibu wa sheria za misitu za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu. Wavunaji hawa huingia wenyewe ama kwa kuonyeshwa na wenyeji wenye ufahamu wa maeneo yenye miti na aidha hawatoi taarifa katika serikali za vijiji ambavyo vinahusika na umiliki wa maeneo hayo.

Kwa mfano:

Zaidi ya mbao 3000 na magogo yalikamatwa katika misitu ya Mtanza – msona , makima, ugezi, mtita, mchungu na maeneo mengi yanayopakana na wilaya jirani, kwa nyakati tofauti. Uchunguzi uliofanyika ulidhihirisha kuwa wenye mbao na wafanyabiashara ni wenyeji wa kutoka wilaya jirani.

### 4.5.2 USAFIRISHAJI/BARABARA

1. Barabara zinazotumiwa kusafirisha mazao ni barabara inayotokea Mloka – Vikumburu hadi Kisarawe.
2. Barabara ndogo zinazotokea misitu ya Ruhoi, Makima hadi kijiji cha Kongwa wilayani Kisarawe.
3. Barabara za msimu/ seasonal roads zinazotoka katika misitu iliyopakana na wilaya ya Rufiji na Kisarawe (misitu ya Mtita na Mkwandara n.k)
4. Barabara ndogo zinazotokea misitu ya Mchungu Kikale na misitu ya wazi ya Kivinja A na Kivinja B hadi Njopeka Wilayani Mkuranga.
5. Usafirishaji mwingine ni wa bahari magogo/mbao na nguzo husafirishwa wilaya jirani.

### 4.5.3 JUHUDI ZINAZOFANYWA NA WILAYA KUZIBA UVUNAJI HUO

1. Juhudi zinazofanywa na wilaya za kuziba uvunaji huo ni za kusimamia sheria (law enforcement) pamoja na kuimarisha sheria ndogo ndogo za Halmashauri ya wilaya na vijiji.
2. **DORIA:** Kuongeza doria katika misitu yote inayopakana na wilaya jirani, pamoja na kutambua barabara zote zisizorasmi na zinazotumiwa kusafirishia mazao ya misitu.
3. Utoaji wa elimu ya ushirikishwaji wa jamii katika kumiliki na kusimamia maliasili.
4. Uanzishwaji wa kamati ndogo za vijiji za usimamizi wa misitu na hifadhi ya mazingira.
5.Uanzishwaji wa misitu ya vijiji.

6.Uanzishwaji wa kamati ndogo za wilaya na kubuni mipango ya usimamizi, umiliki na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu wilayani Rufiji (Rufiji action and harvesting plan task force)
7.Wilaya kwa kushirikiana na miradi iliyopo ya kuhifadhi mazingira, imekuwa ikiendesha semina na warsha kwa viongozi na wataalam wa aina mbalimbali kuhusu umuhimu wa kushirikisha jamii katika kusimamia na kumiliki maliasili wilayani Rufiji pamoja na kufafanua sera na miongozo ya ushirikishwaji jamii katika kusimamia maliasili kama njia pekee ya kudhibiti uvunaji holela, uharibifu wa misitu na matumizi endelevu ya maliasili Wilayani Rufiji.

### 4.5.4 MAFANIKIO

1.Kasi ya uharibifu na utoroshaji wa mazao ya misitu imepungua kidogo, kutokana na doria za mara kwa mara katika misitu na maeneo yanayopakana na wilaya jirani.
2.Mipango ya ushirikishwaji jamii katika kusimamia na kumiliki mali asili imekwishaanza katika vijiji vya MTANZA, MSONA na MBUNJU MVULENI. Mpango huu utaendelezwa katika vijiji vyote vinavyopakana na msitu wa hifadhi wa Ngumburuni.

**Wataalam**
Maafisa misitu 2 na Forest Assistant 2 wameajiriwa na wilaya pamoja na serikali kuu kupunguza tatizo la uhaba wa watendaji katika idara ya misitu.

### 4.5.5 VITENDEA KAZI

Wilaya imepata gari moja jipya kwa ajili ya kazi za doria.

### 4.5.6 FEDHA ZA DORIA

Kiasi cha Tshs 1,500,000 zilitolewa na wizara kuimarisha kazi za doria wilayani Rufiji.

### 4.5.7 SABABU ZINAZOSABABISHA KUSHINDWA KUZIBA UVUNAJI HUO

1.Jamii haijaelimika au kupata ufahamu wa kutosha kuhusu kusimamsia na kudhibiti uvunaji holela katika vijiji vyao.
2.Mpaka kati ya wilaya ya Rufiji na Kisarawe haueleweki vizuri na kusababisha kuongezeka kwa uharibifu wa misitu iliyoko mpakani na wilaya jirani.
3.Hakuna utaratibu wa mawasiliano kati ya wilaya zote za jirani kuhusu kushirikiana katika kudhibiti uvunaji holela na uharibifu wa misitu inayopakana na wilaya zetu pamoja na doria ya mazao yanayovunwa na kutoroshwa nje ya wilaya yoyote jirani.
4.Uchache wa wataalamu kulinganisha na ukubwa wa wilaya.
5.Uchache na ucheleweshwaji wa fedha za kufanyia doria zitolewazo na wizara katika wilaya (Retention Fund).
6.Kuwepo kwa barabara nyingi na zisizo rasmi zinazotoka wilayani Rufiji na kuingia wilaya jirani pamoja na wilaya kushindwa kuweka vizuia katika njia hizo.
7.Tatizo la uharibifu wa misitu na uvunaji holela bado halijaonekana kuwa ni tishio kwa jamii ya wilaya ya Rufiji. Aidha jamii haijapata ufahamu na uelewa wa kutosha kuhusu wajibu wao wa kushiriki katika kusimamia na kumiliki misitu kisheria.
Katika hali hii uvunaji umekuwa ukifanyika kiholela katika maeneo yote ya wilaya na idara ya misitu ikiwa ndio chombo pekee kinachotegemewa katika kudhibiti hali hii.
8. Umasikini (poverty) na ukosekanaji wa ajira mbadala katika jamii unachangia kwa kiasi kikubwa kwa jamii kushiriki katika uvunaji holela na usafirishaji wa mazao ya maliasili kinyume ba taratibu na sheria.

## 4.6 Kiambatisho Namba 6: Taarifa Ya Idara Ya Maliasili Wanyamapori Wa Ya Rufiji

**Utangulizi:**

Uhifadhi wa wanyamapori nchini huzingatia sheria Na. 12 1974, sera ya Wanyamapori 1998.

### 4.6.1 MAENEO MAARUFU YA WANYAMA PORI WILAYA YA RUFIJI

- Pori la Selous (6,258km$^2$)
- Eneo la kijiji cha Ngarambe (22,579ha), Tapika (54,143ha) kutokana na sorovea ya matumizi ya ardhi 2001
- Mtanza msona hadi Mloka (Haija pimwa)
- Maeneo mengine Mto Rufiji, Mhoro, Maziwa n.k

### 4.6.2 TAASISI ZISIZO ZA KISERIKALI ZINAZOSHIRIKIANA NA IDARA

| S/no. | Taasisi | Eneo |
|---|---|---|
| 1 | WWF. TZ Programu ofisi | SGR Kanda ya Kaskazini Mashariki<br>Vijiji vya Ngarambe na Tapika |
| 2 | GTZ/SCP<br>(Selous Conservation Programme) | SGR<br>Vijiji vya Ngarambe na Tapika |
| 3. | REMP (IUCN) | Eneo la tambarare na ardhi la mto Rufiji, Mhoro na Delta ya Rufiji<br>Vijiji 4 I.e Mtanza msona, Mbunju mvuleni, Jaja na Twasalie |

### 4.6.3 Uvujaji Wa Maliasili

- Ujangili wa wanyamapori na nyara za serikali, maeneo ya SGR, vijiji vya Kilimani-Mloka, Nyamwage, Mhoro, Mbwara, Tawi, Kitapi, Kiwanga, Kiboko Ikwiriri. Baadhi ya majangili hutoka wilaya ya Kisarawe, Mkuranga, Kilwa na Dar es Salaam.
- Njia zitumikazo ni za Barabara ya Kilwa, Kibiti –Dar; Mloka -Kisarawe-Dar; Mloka –Kibiti-Dar; Mhoro-Rufiji- Delta bahari ya Hindi
- Njia za Baiskeli-Rufiji- Mkuranga/Kisarawe-Dar;Rufiji-Kilwa
- Njia za Miguu
- Wawindaji Halali wanaokata leseni Kisarawe na kuwinda eneo la Mkigula/ Mloka (Rufiji) hivyo kumekuwa na mgongano
- Kumekuwa na msongamano wa uwindaji katika sehemu moja (Julai-Desemba)

**MIKAKATI ILIYOCHUKULIWA NA IDARA KATIKA KUZIBA MIANYA.**

- Kuendeleza uhifadhi kupitia jamii iliyopo karibu na maeneo ya hifadhi
- Doria dhidi ya uhalifu kwa kushirikiana na SGR na KDU n.k
- Uimarishaji wa viziui vya maliasili
- Uanzishaji hifadhi za wanyama pori za vijiji
- Kusaidia vijiji kutunga sheria ndogo
- Kubuni miradi mbadala inayowasaidia wananchi katika kuongeza kipato

- Askari wa hifadhi hufanya doria zao
- Kamati za mazingira vijijini zimeundwa kusimamia mazingira

### 4.6.4 BAADHI YA MATATIZO YALIYOJITOKEZA

- Fedha kidogo zinatengwa na Halmashauri katika kuendeleza uhifadhi wa wanyama pori
- Uchache wa watumishi
- Uchache wa vitendea kazi
- Pingamizi kutoka chama cha wawindaji Tanzania i.e HAT kwa dhana ya kushirikisha jamii (CBC)

**MIKAKATI MINGINE KATIKA KUBORESHA UHIFADHI WA WANYAMAPORI NA MAZINGIRA.**

- Kushirikisha vijiji vingine katika hifadhi hasa vile vilivyopo karibu na SGR
- Kutatua migogoro iliyopo baina ya Vijiji na Hifadhi
- Kuendelea kushirikisha jamii katika kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyama
- Kuendelea doria kwa kushirikiana na wahifadhi
- Kutoa elimu za wahifadhi
- Kuimarisha vizuia vya maliasili
- Serikali na Halmashauri kutenga fedha za kutosha
-

## 4.7 Kiambatisho Namba. 7: Halmashauri Ya Wilaya Ya Mkuranga

**TAARIFA FUPI YA KUHIFADHI MALIASILI ZA WILAYA YA MKURANGA KATIKA WARSHA YA UJIRANI MWEMA – RUFIJI TAREHE 03 –04/12/2002**

### 4.7.1 UTANGULIZI

Wilaya ya Mkuranga ni moja kati ya wilaya sita katika mkoa wa Pwani.

Wilaya imebahatika kuwa na maliasili nyingi ambazo bado hazitumiki kikamilifu katika kuondoa umasikini wa wananchi wake. Maliasili zilizopo wilayani ni kama bahari ya Hindi, mito, mabwawa, misitu, wanyamapori, samaki, madini (chumvi na mchanga) na ardhi.

Wilaya inapakana na jiji la Dar es Salaam hivyo maliasili za wilaya hii hutegemewa sana na wakazi wa Dar es Salaam. Sehemu kubwa ya manufaa ya kiuchumi kutokana na maliasili huwanufaisha wafanyabiashara wa Dar es Salaam, lakini sehemu kubwa ya madhara kutokana na matumizi yasiyo endelevu ya maliasili hizi huwakumba wananchi wa Mkuranga mfano mafuriko, ukame, kimbunga, umasikini na uharibifu wa mazingira.

Wilaya inajitahidi kukabiliana na uharibifu wa maliasili zake kwa kushirikisha wadau wote ndani na nje ya Wilaya. Umeahidiwa mpando wa miaka mitano 2001 – 2005 wa kuhifadhi mazingira ambao unahusisha upandaji na utunzaji wa miti, kilimo mseto, uhifadhi wa ukanda wa pwani wa bahari ya Hindi, kutoa elimu juu ya matumizi endelevu ya mali asili zetu na kusimamia vyanzo vya maji.

Katika juhudi za kuelimisha jamii, wanavijiji wamepata mafunzo mafupi ya uhifadhi misitu kwa mbinu shirikishi (J.F.M), kilimo cha mwani, uchimbaji mabwawa ya kufugia samaki wa maji baridi na wa baharini, na utunzaji mikoko.

Kasi ya upandaji miti inaongezeka kwa kushirikisha wananchi katika kampeni ya upandaji miti ya kila mwaka, na pia kwa njia ya kushindanisha washiriki mbalimbali katika mpango wa C.E.A.S.

### 4.7.2 MIRADI INAYOSIMAMIA MALIASILI

1. TCMP/1.C.M (Integrated Coastal Management) – uhusika na uhifadhi mazingira ya pwani
2. AMREF – Unahusika na usafi wa mazingira na maji salama
3. CEAS – (Coastal Environment Award Scheme) – unahamasisha uhifadhi mazingira kwa kushindanisha washiriki mbalimbali.
4. HPI – (Heifer Project International) – unahusika na uhifadhi mazingira – kilimo mseto.
5. Hivi sasa WCST na SONGAS wana mpango wa kuanzisha shughuli zao za uhifadhi mazingira.

### 4.7.3 MASUALA YA UKUSANYAJI WA USHURU

Ukusanyaji ushuru/ada Wilayani Mkuranga unafanywa na mawakala kwa ushuru/ada ya Halmashauri katika maeneo yote ya misitu na samaki. Ada/ushuru wa serikali kuu hukusanywa na watumishi wa idara /sekta husika kwa niaba ya katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii.

### 4.7.4 MIKAKATI YA WILAYA DHIDI YA MATUMIZI HARIBIFU YA MALIASILI

1. Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa maliasili zetu ikiwa ni pamoja na kuelimisha jinsi ya kutumia maliasili kwa busara, mfano kutumia majiko sanifu.
2. kusimamia uundaji Kamati za Mazingira za vijiji.
3. kushirikisha jamii katika uhifadhi wa maliasili ikiwa ni pamoja na kufanya doria za pamoja.
4. kuandaa mpango wa hifadhi maliasili kuanzia ngazi za vijiji, kata hadi wilaya kulingana na sera za taifa.
5.kutunga sheria ndogondogo na kuzitumia kuwabana wakorofi.

6.kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi – kutenga kwa ajili ya shughuli mbalimbali.
7.kusisitiza njia mbadala za kupatia kipato badala ya kutegemea maliasili tu mfano W. C. S. T. wameahidi kutoa mikopo kwa vikundi vya uzalishaji mali vijiji vya Kibudu na Kibuyuni.
8.kufuata njia za kilimo cha kisasa (kutumia mbolea, kutumia mbegu bora, kuacha kilimo cha kuhamahama n.k)

### 4.7.5 MASUALA YENYE UTATA NA JINSI YA KUYATATUA

| SUALA LENYE UTATA | UFUMBUZI |
|---|---|
| (1) Kudhibiti uvunaji holela | -Wizara, Wilaya na jamii kwa jumla kuweka mipango ya matumizi endelevu ya maliasili.<br>-Kushirikisha jamii kuhifadhi Maliasili |
| (2) Maingiliano ya kikazi, kiidara na kiwizara | - Mipango ya maendeleo ishirikishe idara/Wizara husika. |
| (3) ukosefu wa vyombo vya usafiri wa baharini na nchi kavu | -Wizara husika isaidie kutoa usafiri inapobidi |
| (4) Ukosefu wa fedha za kutosha | - Wadau wachangie shughuli za uhifadhi. |
| (5) Mgawanyo wa faida tokana na Maliasili | - Jamii zipate manufaa ya Kiuchumi, kulingana na uvunaji wa maliasili zao. |
| (6) Mipaka kutofahamika vizuri. | - Mipaka ya kiutawala ya Wilaya na Wilaya, vijiji na vijiji itambulike ardhini kwenye ramani. |

### 4.7.6 MBINU ZA PAMOJA ILI KUTATUA MATATIZO YA WILAYA KATIKA

KUHIFADHI NA KULINDA MALIASILI

1. Kuandaa semina na warsha za pamoja (ujirani mwema) mara kwa mara ili kuelimishana na kufahamishana juu ya Uhifadhi maliasili.
2.kupeana taarifa za kazi kila robo mwaka
3.kushirikiana kiwilaya katika kufanya doria kwenye maliasili zilizopo mpakani.
4.kupeana taarifa za matukio yasiyo ya kawaida mfano utoroshaji wa maliasili toka wilaya moja kwenda wilaya nyingine.
5.kutoa motisha kwa anayetoa taarifa za kuokoa utoroshani /uvunaji holela maliasili.
6.kuwepo na utaratibu wa mashindno ya uhifadhi mazingira Wilaya kwa Wilaya.

### 4.7.7 JINSIA NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

1.Wilaya inajitahidi kuhamasisha jinsia zote zishiriki sawa katika kusimamia mazingira.
2.Wilaya inatilia mkazo msamaha wa kulipia leseni za utandaji samaki baharini hususani kwa akina mama.
3.jinsia zote zimeruhusiwa kuvua samaki kwa kutumia ndoana tokea nchi kavu.
4.Wilaya kwa kushirikiana na mradi wa TCMP unashindanisha jinsia zote.

**KUANZISHA MTANDAO WA HABARI NA KUKUBALIANA MBINU ZA KUSHIRIKIANA.**
1.Kuanzisha kijarida kinachoelezea shughuli za uhifadhi mazingira Mkoani.
2.Kupeana taarifa za uhifadhi mazingira kwa vipindi maalum mfano, kila robo mwaka.
3.Waandishi wa habari wa Wilaya wakutane angalau mara mbili kwa mwaka na kupeana habari za mazingira.

## 4.8 Kiambatisho Namba 8: Maelezo Mafupi Kuhusiana Shughuli za Hifadhi ya Bahari Mafia (MIMP)

**KATIKA WARSHA YA JIRANI MWEMA KATIKA UKUMBI WA FDC RUFIJI TAREHE 3-4 DESEMBA 2002WILAYA YA MAFIA**

**1.0 UTANGULIZI**

Hifadhi ya Bahari Mafia, ilianzishwa rasmi mnamo mwaka 1995 kwa sheria namba 29 ya mwaka 1994. Sheria ya Hifadhi za Bahari Maeneo Tengefu, Tanzania. Hifadhi hii imejumuisha vijiji 11 katika eneo hili la Hifadhi vimo visiwa vidogo vidogo vinne navyo ni Chole, Juani, Jibondo na Bwejuu. Eneo ni km 822.

Hifadhi hii ipo Wilayani Mafia na ipo kilomita 160 kusini mwa Dar es Salaam, na kilometa 20 kutoka usawa wa Mashariki mwa kapa ya mto Rufiji.

**2.0 MADHUMUNI YA HIFADHI**

i.Kulinda kuhifadhi na kudumisha viumbe na uoto wa baharini na nchi kavu, pamoja na mifumo ya ikolojia ya baharini na pwani.

ii.Kusimamia maeneo ya bahari ukanda wa pwani, pamoja na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu wa rasilimali zilizopo, pia kuwezesha rasilimali zilizovunwa kupita kiasi kurejeshwa au kukarabati mifumo ya ikolojia iliyoharibika.

iii.Kuhakikisha kuwa vijiji na wakazi wengine katika vijiji jirani au wanaotegemea Hifadhi ya Bahari wanashirikishwa kwa ukamilifu katika hatua zote za mipango, maendeleo na usimamizi wa Hifadhi, wananufaika na faida za uendeshaji, pia wanapewa kipaumbele katika matumizi ya raslimali na fursa za kiuchumi zinazotokana na kuanzishwa kwa hifadhi ya Bahari.

iv.Kuchangia matumizi ya raslimali ambazo hazijatumika ipasavyo kama vile uvunaji kaa na chaza n.k

v.Kuhifadhi na kulinda makumbusho ya kihistoria, magofu na raslimali nyingine za kitamaduni ambazo zimeainishwa kuwa ni muhimu katika historia ya kisiwa cha Mafia, na kutoa fursa ya uendeshaji unaofaa wa utalii endelevu.

**3.0 LENGO LA HIFADHI YA BAHARI MAFIA**

Lengo la Hifadhi ya Bahari Mafia, ni kuhifadhi raslimali zote za kimaumbile na za kibaolojia ili ziweze kuendelea kunufaisha na kutumiwa kiuzalishaji na vizazi vilivyopo na vijavyo.

**4.0 MUUNDO**

4.1 Bodi ya Wadhamini – Taifa
4.2Kamati ya Ushari – Wilaya
4.3Kamati za Hifadhi – Vijijini

**5.0 RASLIMALI**

5.1 Viumbe mbalimbali wa baharini kama vile samaki, kamba, kaa, chaza, pweza, ngisi pamoja na kasa.

5.2 Misitu ya mikoko, kuna aina ya mikoko mikoko ifuatayo Mkoko (Rhizophora), Mkandaa (ceriops), Mchuu (Avicennia), Msinzi (Bruguira) na mpira (Sonneratia), pia Mkomafi (Xylocurpus)

5.3 Msitu wa Mlola, msitu huu ni miongoni mwa misitu michache ya asili katika ukanda wa pwani iliyobakia. Msitu huu una aina mbali mbali ya miti na wanyama wadogo wadogo pamoja na ndege, nyoka n.k.

5.4 Fukwe: kuna fukwe nzuri ambazo hazijachafuliwa sana ukilinganisha na sehemu nyingine.

**6.0 CHANGAMOTO KWA HIFADHI YA BAHARI MAFIA**

6.1 Matumizi ya nyavu za kuvuta na zenye macho madogo (mtando)
6.2 Msongamano wa wavuvi kutoka nje na Mafia kama vile Mtwara, Dar es Salaam Zanzibar.

6.3 Uchomaji moto ovyo.
6.4Ukataji miti kiholela
6.5Uvunaji wa matumbawe baharini
6.6Uanzishwaji wa viwanda vya kusindika na kusafisha samaki.

**7.0 HATUA ZINAZOCHUKULIWA**
7.1 Kutoa elimua ya mazingira kwa mavuvi, wananchi, na wawekezaji wengine
7.2 Kuendesha doria
7.3 Kugawa maeneo ya matumizi katika kanda
Kanda tegefu (core zone) sehemu hii hairuhusiwi uvunaji wa aina yoyote isipokuwa shughuli za kitalii na utafiti.
Kanda ya matumizi maalum (special use zone); sehemu hii uvunaji unaruhusiwa kwa wakazi waliopo ndani ya eneo la hifadhi tu na kwa mitego Fulani Fulani kama vile mshipi, madema, wando au uzio.
Kanda ya matumizi ya jumla; sehemu hii wavuvi kutoka nje ya eneo la Hifadhi wanaruhusiwa kufanya shughuli zao ili mradii waombe kibali kwa Mhifadhi Mfawidhi kupitia Kamati za Hifadhi na serikali za vijiji. Mitego inayoruhusiwa ni kama ile ya kanda ya matumizi maalum kuongeza na nyavu za Jarife na nyavu za kupweleza.
7.4 Kuanzisha mpango wa kubadilishana mitego kuchukua ile haribifu na kuwapa wavuvi ile mitego endelevu.
7.5 Kwa kushirikiana na wanavijiji kubuni njia mbadala za kiuchumi kama vile kilimo cha mwani, ufugaji wa nyuki, samaki na kilimo cha mazo ya biashara kama vile korosho, ufuta na alizeti.

## 4.9 Kiambatisho Namba. 9: Mafia District Council Description of Mafia Natural Resources Utilisation

- Geographical History

Mafia Island is situated to the East Coast of the Tanzania /coastal line 160 km from Dar es Salaam. The District total area is 1,728 square kilometres, including water. The land itself is 518 square kilometres i.e the big Island and its Islets. The remaining part is water body which covers an area of 1,210 square kilometres. Mafia district comprises the big Island called Mafia mainland and other 4 small Islands inhabited by people namely Juani, Jibondo, chole and Bwejuu. Also there are Miewe, Mbarakuni, Nyororo and Shungimbili Inlets, which are fisher camps as well as Travel stop over during rough sea conditions.

- **Natural Resources Status.**

#### 4.9.1.1 Forestry

Mafia District has two types of forest i.e Forest Reserves and Community Forests.

(a) Forest Reserves

(i) Low land Coastal forest (inhambane) which is called MLOLA Forest Reserves. The total area is 125.2 h, part of it 50.2 ha is under the district Forest Reserve and the other part 75 ha is the Government Forest Reserve managed by Mafia Island Marine Park – MIMP.

(ii) Mangrove forest have the total coverage of 404.5 h and form patches around Mafia District area, but mangroves are very dense at Ras-Kisimani, Chole bay and Kirongwe – Kanga rivers. These reserves are under supervision of Mangrove project. The above types of Forests are Natural.

(b) Community Forests.

The 3 forests namely Kilombero Community forest, Mwamizi Community Forest and Jimbo Community Forest. The District is trying in lieu of conservation to change the Forests from Community Forest to District Forest Reserves but still be managed by the Community at the area and they continue to be Community Base Management Forest, which the implies to Mloka District Forest Reserve. Generally Mafia forests contribute much to the rainfall available in Mafia.

(b) Fisheries

Mafia District marine waters in worldwide known for its richness in fishery biodiversity and scientifically was approved and hence the first Marine Park in Tanzania were established (1994) i.e Mafia Island Marine Park.

Among the fishery species of the World, Mafia waters contributes a lot, but collectively you can find sperm whales, turtles, cephalopods, Dolphins, Beche-de-mer, Dugongs, crustaceans, bone fishes, Cartilaginous fishes, starfishes, sea urchins, Sea anemones, Sea weeds, Corals and fringes.

Fishery industry leads second to agriculture this attributes to the Mafia peoples income, of course the great number of fisher folk are the artisan fisher. For example the number of fisher fold in 1999 was 3194, using Ngalawa, Mashua, Mitumbi etc. amounting 688 vessels; they catched 5,800.72 metric tonnes, valued 728,400,000/= Tanzania Shillings. The types of gear used were Nets 699, lines 1022, trapes 1076, ring nets 8 and shark nets 495. Data's are as follows below:-

| YEAR | RESOURCE | WEIGHT (M.TONS) | VALUE TSHS '000' |
|---|---|---|---|
| 1999 | Fish (Domestic) | 5,500 | 5,500.00 |
| | Beche-de-mer | 18.39 | 18,390.00 |
| | Lobsters | 18.70 | 56,100.00 |
| | Octopus | 248.90 | 96,560.00 |
| | Squids | 14.73 | 7,350.00 |
| | **Total** | **5,800.72** | **728,400.00** |

We anticipate that 300.72 Metric tons were exported to international market thus boosting National economy growth.

The District is praising the Government in its effort to minimize (but in our area to stop) Dynamite practices of fishing which in turn the fishery industry shows an increase in fish production. In this the district also appreciate the strong hand on enforcement with regard to conservation which is owned by the Management of Mafia Island Marine Park to slow down the illegal fishery in our District as well as introducing alternative fishing gears, awareness and stake holders capacity building.

- **Wildlife**

Among Wild animals found in Mafia are the Dikdik, Hippotatumus, Fruit bats, Pigs, Black monkeys, snakes and variety of birds e.g egrets. There are swamps which serve the life of Hippos.

- **Bee Keeping**

Mafia Island has flowering shrubs and trees which attracts insects like Bees and in turn enhance the honey and wax production. Mafia Island Marine Park is well involved in the aspects by providing equipments (bee hives, uniforms) as well as education to local people in the areas. Still the wax and honey production is low and strategies are under way to improve the situation.

- **Antiquities.**

The Mafia history can be traced back from the people themselves as well as from the ruins available e.g Kua in Juani, Chole ruins, Kanga ruins, Kisimani Mafia submerged town etc.

- **Beaches**

The total length of Mafia Main Island and it small Island and Islets beaches is 188 km by estimation, 82% out of that is a very beautiful white sand; the remaining 12% contributes to snerio of mangroves trees, sand bags and coral rags. There are also 4 Tourist hotels, which are situated along the beaches.

Natural Resources found in Mafia

- forest, Marine fishes and freshwater fishes
- corals, sea grasses and sea weeds
- wild animals
- bees, birds and snakes
- livestock
- sand bags and beaches
- Antiquities eng ruins and caves
- Ocean and swamps

- **Project which deals with Natural issues**

Conservation

-Mafia Island Marine Park (MIMP)

-Turtle and Dugongs Conservation Programme (Sea Trust/WWF)
-Low land coastal Forest (WWF)
-Mangrove forest Project (NORAD)

- **Destruction of Natural Resources**

Strategies

- **Patrols to sensitive areas e.g Okuza and Nyuni Islets (Kilwa), Dima and Kibanju (Rufiji), Kwale and Koma (Mkuranga).**
- **Awareness reach to areas mentioned above i.e use of posters and T-shirts also award scheme.**
- **Supply of proper gear to fishers e.g in Rufiji Delta by Tanpesca Kanga, Bweni by other small companies.**
- **Monitoring of fisher folk e.g migration from one area to another through inspection and valid permits from authorized officers**

- **Controversial issues**

Boundaries of licensing officers i.e illegible officers to take actions in neighbour district (Joint operations).

- Less power in controlling and Monitoring of Natural Resources licences issued by sister Ministry e.g Trawlers licence issued by fisheries headquarters (zoning system).

- **Problems**

  -Absence of patrol boats. For the sake of conservation and sustainable exploitation the district requires a durable fibre boat complete with simple navigation aids to cater the enforcement sector.

  -Operation cost. The district alone cannot afford I because of huge area of water bodies (sq km 1210) which is 70% of the total area of Mafia district.

- **Improper, harvest of Natural Resource through…**

- Use of unsustainable fishing gears
- Clearing of indigenous tree species e.g Minywamaji, Mziwati, Mchati, Mbura etc. especially on catchment areas.
- Disturbances of breading sites e.g fruits bats, birds, (coral reef egret), Hippotatumus, pigs, fish etc.

- **Geographical barrier**

- High cost to bring officers/experts from neighbour districts
- Unreliable communication system, telephone, radio call, electronic etc.
- Marine transport, absence of jetty, ship.

- **Poverty**

- Poor fishing gear
- Illiteracy
- Pesticides, recycling, Natural Resource residues – Proper uses
- Few/No extension officer
- High post harvest losses –logs, fishes, trees etc.

- Fund allocation from central Government e.g retention Fund from export of Marine Production.

- **Solution**

- All stake holders to plan together implement, monitor and evaluate
- To provide simple credit facilities to stake holders
- To continue with education and awareness programs
- To have a joint government operations
- Ministry of Natural resources to disburse our share (Retention) accordingly.

- **Gender issues**

How Mafia women's participate in the Natural resource utilization

- Octopus fishery
- Sea weed farming
- Transport of processed fish (fried fish)
- Beche-de-mer/shells fishery
- Raffia produces
- Poes collection and sells
- Retail charcoal business
- Fire wood collection and sells

The women's are involved in village to district level environmental Committees.

- Communication system among District
  Equipments
- VHF land base radio

**Strategies**

- Initiation of zone news paper
- Use of Television and radios available
- Exchange quarterly report
- Meetings, seminars or workshops

## 4.10 Kiambatisho Namba 10: A Brief Presentation on Leakage of Natural Resources (Mangroves)

**GOOD NEIGHBOURS OF RUFIJI "WORKSHOP/MEETING" A BRIEF PRESENTATION ON LEAKAGE OF NATURAL RESOURCES (MANGROVE LEAKAGE)**
**PREPARED BY MANGROVE PROJECT CENTRAL ZONE, IKWIRIRI, RUFIJI 03/12/2002**

**1. INTRODUCTION**

The Mangrove Management Project 9MMP) which is under the Ministry of Natural Resources and tourism in the Forest and Beekeeping Division 9FBD) is an institution empowered to manage the Mangrove Forest Reserve of mainland Tanzania. The overall development goal of the project is to enhance the contribution of the mangrove ecosystems to the economy of the country by rational utilization of mangrove ecosystems on a sustainable basis.

In Tanzania, mangrove occur along the coastline of about 800 km from the border with Kenya in the North to that of Mozambique in the South and around the Islands off the coast. According to 1989 inventory (MTNRE, 1991) the mangrove forests of mainland Tanzania cover a total area of about 115,500ha.

Administratively, the Rufiji delta falls in the boundaries of the Rufiji district in the Coast Region, Tanzania.

The total area of mangrove forests in the Rufiji delta is about 53, 200 ha equivalent to 46% of all mangrove forests in Tanzania. The length of the Delta is 65 km with an average maximum width of 25 km. The extent of the Delta area is wide enough to favour linkages with neighbousing District.

However, the more closely linkage is the boundary of Rufiji and Kilwa District in the south. In the east the Delta is linked to Mafia District by the Indian Ocean. In the North the Delta area is linked to Mkuranga district both by the Indian Ocean and the mainland.

**2. LEAKAGE OF MANGROVES**

Leakage of mangrove through illegal mangrove cutting is one of the management problems of MMP central zone.

According to the management plan for the mangrove ecosystem of Mainland Tanzania, all the mangroves in this country have been classified into zones as one of the management strategies to achieve management objectives.

These are protection, production, recovery and Rehabilitation and development zones.

The production zones are ecologically stable areas with sufficient regeneration potential that permits controlled harvesting. The Rufiji delta has many areas falling under this category.

However, the management plan for the mangrove ecosystems of Mainland Tanzania was prepared more than 10 years ago. This means that at present some of the recommended uses in the mangrove zones are at variance with what was recommended uses in the mangrove management plan (1991). It is obvious that there are a lot of changes that have taken place in the 11 years period since 1991.

As regards to the Forests (amendment) Rules, 2001 the fees for the mangrove poles are as follows.

| **Class** | **Diameter at butt** | **Rate per Score Tshs.** | **Rate per Pole** |
|---|---|---|---|
| Class I | 15-20 cm | 6,000.00 | 300.00 |
| Class II | 10-14.9 cm | 4,000.00 | 200.00 |
| Class III | 5-9.9 cm | 2,000.00 | 100.00 |
| Class IV | Below 5 cm | 1,000.00 | 50.00 |

All mangrove trees of over 20 cm diameter overbark at 1.3 metres above ground shall be considered as logs and fees will be 40,000/= per $m^3$.

However, some unfaithful mangrove trades escape from paying these fees for the mangrove poles and logs as a result of that the government is loosing substantial amount of revenue.

Leakage of mangrove in the Rufiji delta can be classified into 4 groups:

(i) Mangrove leakage done by the Rufiji delta villagers to Mafia, Dar es Salaam, Zanzibar and other neighbouring areas/business centres.
(ii) Leakages as a result of businessmen and women from outside Rufiji to Mafia, Dar es Salaam, Zanzibar and other neigbouring areas/business centres.
(iii) Mangrove leakage done by unfaithful traders carrying/transporting poles in their vessels more than what have been permitted in the licence.
(iv) Leakage engineered by the boundary conflicts between Rufiji and Kilwa districts has not been found.

Despite the fact that there are many ecologically stable areas in the Rufiji delta that permit controlled harvesting, the extent of mangrove leakage is not very high.
The most common type of mangrove leakage in the Rufiji delta is the cheatful information given by the businessmen about the exact amount of poles. That is to say about 50% of the mangrove poles are stolen this way by these unfaithful traders.

## 3. MEASURES TO CONTROL LEAKAGE OF MANGAROVES

The second most important management strategy of MMP to ensure adequate management of mangrove ecosystem in Tanzania is to increase involvement and awareness of local communities in mangrove ecosystem.

### (i) Formulation of VNRCs and village meetings

The project strengthens participation of local communities through VNRCs. VNRCs act as a link between the Ministry of Natural Resources and Tourism through MMP and the villagers. The Project provided guidelines on formulation of VNRCs. Meetings are further conducted regularly to discuss various issues pertaining to mangrove conservation.

Meetings are regularly conducted where the mangrove officers receive different reports from villagers, and suggestions to improve mangrove conservation. Meetings are conducted regularly to discuss various issues pertaining to mangrove conservation.

Meetings are regularly conducted where the mangrove officers receive different reports from villagers, and suggestions to improve mangrove conservation. Meetings are conducted after every second month.

The VNRCs so far formulated are active in the following activities.

- VNRCs organised patrols
- Report writing
- Law enforcement
- Record keeping
- Extension service to the rest of the community
- As informers
- Other forest activities like planting, etc.

The main activities under this output are:

(i) Participatory Rural Appraise (PRA)
(ii) Formulation of Village Natural Resources Communities (VNRCs) AND VILLAGE MEETINGS
(iii) Joint patrols in mangroves
(iv) Artificial and natural regeneration of mangroves
(v) Harvesting supervision
(vi) Extension services in schools

**(ii) Participatory Rural Appraisal (PRA)**

Local communities living adjacent to mangroves are expected to take an active role in the conservation and management of mangrove forests, but there is a scanty knowledge on their socio-economic life PRA is therefore conducted to achieve the following objectives:

- Determine needs of both male and female villagers in mangrove ecosystems;
- Exploiting best strategies and methods of mangrove management
- Developing plans of involving communities in mangrove management
- Tapping tradition knowledge from communities in managing mangrove ecosystem;
- Improving management plans

**(iii) Joint Patrols in Mangroves**

This activity is done in collaboration between MMP staff and VNRCs to check for illegal activities in mangroves.

According to VNRCs regular reports on illegal activities including leakage of mangrove from the delta have been reduced significantly.

**(iv) Artificial and natural regeneration of mangroves**

Artificial generation through mangrove planting is done in open areas. Open areas may be due to rice cultivation, charcoal making or any other causes. In rice farms, planting is done where the owner of the plot is given responsibility to take care of the planted mangroves. When the canopy of mangroves expands rice farming stops, and the area is left for mangroves to grow.

Natural regeneration is always observed in the mangrove reserve as a result of sediment deposition and protection of activities involving depletion of mangroves.

The extent of area so far naturally regenerated has not yet been estimated though there are some evidences of natural regeneration. Plans are underway to resurvey the mangrove area.

**(v) Harvesting supervision**

Harvesting of mangrove poles is allowed in development zones. Poles of class 4 and 3 and more preferred, i.e below 5cm and 5.1-cm DBH, respectively, which are sold in scores (20 poles per score).

VNRCs and MMP staff do supervision jointly. The procedure is that, the MMPA staff identifies sites suitable for harvesting. A customer is supposed to go through the VNRCs and Village Executive Officer (VEO) before she/he gets a licence from MMP staff or block i/c. the Block i/c collects Central government revenue, while VEO collects District Council revenue and the VNRCs collects village revenue as levy.

Finally the Block i/c issues a transit pass which goes back through the same stages to the VNRCs as the permission to transport the poles.

The VNRCs in 24 village in the Rufiji delta are activity responsible to observe the harvesting procedures where the customers have to consult VNRCs before the mangrove officer offers as harvesting licence. Through this supervision about 10 Tshs. Mill. Has been collected from mangrove sales as poles during the financial year 2001/2002 compared to the amount of Tshs. 7 Mill. And TAS 9 Mill. Collected in 1999/2000 and 200/2001 respectively.

**(vi) Extension Services in Schools and villages**

Success of mangrove management will depend among things on effective two-ways communication between the MMP staff and the coastal villagers. This is done through sensitization of the entire community on mangrove conservation and related ecosystems.

In primary schools, this is done by implementing a special primary schools teaching curriculum while for the villagers as a whole is done through interactive video and cinema shows and radio programmes.

Other measures taken by MMP to control leakage of mangroves include to conducting of seminar on strengthening of revenue collection from the mangroves of the Rufiji delta. The 2 seminars that were conducted in Nyamisati and Mohoro in May 2001, involved all the important stakeholders of mangroves in the entire Rufiji district.

The impact of the two seminars was the dramatic increase in the revenue collected for both central government and local government. Forexample in April, 2001 a total revenue of Tshs. 147,000/= was recorded in the Kwale checkpoint from the Rufiji district council alone in 20 vessels. At the same time a total of Tshs. 660,000/= was record from the same checkpoint for the month of June in about the same number of vessels, an increase of about 5 times the previous record. These mangrove poles and a rogs transported from the Rufiji delta through Kwale checkpoint in Mkuranga district to Dar es Salaam and Zanzibar.

There are allegations that some businessmen escape from paying the government revenue because the selling price of mangrove poles in Zanzibar has been going down each time and sometimes it takes several months before they get paid. They also complain of high costs they incur from cutting of the poles and transportation.

It has once been reported by VNRC (Pombwe village) that some traders, harvesters harvest mangrove poles from their using licences issued in Kilwa. This case revokes the laid down rules by MMP central zone (esp. Rufiji) (See V).

May I pose this as the challenge to Kilwa forest officials to restrict their licenses in Kilwa mangrove forests in order to refuse the above mentioned management problems.

- ❖ The use of chainsaws in felling mangrove poles in ilifriendly to the natural mangrove ecosystem. It has recently been noted that loggers with licences from Kilwa have invaded Pombwe village

mangrove areas. May I still challenge the Kilwa Forest Officials to alert their licensees to stop this or at least help us to alert them for a quite mangrove ecosystems.

❖ Mafia experience shows that some people have residence both in Mafia and Rufiji (esp. Delta dwellers). This interrelationship favours the transfer of products between the two areas.

❖ The mangrove ecosystem products suffer from the consequence of the interrelationship.

❖ In order to control the transfer of the products, there should be strong tie between the respective officials of the two Districts.

❖ If strong legal measures are taken against illegal transfer of the products (eg. Mangrove poles) in Mafia District, the agents of transfer will consequently follow the rules and regulations in Rufiji District.

❖ Mkuranga case shows that it is one of pathways for the transfer of mangrove ecosystem products to Dar es Salaam and Zanzibar.

❖ The mangrove ecosystem products should have special permits from respective authorities i.e

- Village (Origin)
- District council
- Central government

❖ Continuous requisition of those authorized permits by Mkuranga officials strictly will create a good habit of agents of transfer to posses all those document which should be obtained from Rufiji official for Rufiji area products.

❖ Effective use of Mkuranga District checkpoints shall greatly enhance the collection of income for District council for its betterment and the nation at large.

❖ Let us al join hands to protect the mangrove ecosystems for generations today and in future

❖ The fragile mangrove ecosystem future is in the hands of Kilwa, Rufiji and Mkuranga District.

**Frank Sima**
**For: ZONAL MANGROVE OFFICER**
**CENTRAL ZONE**

## 4.11 Kiambatisho Namba. 11: Taarifa Ya Wilaya Ya Kisarawe

**WARSHA YA UJIRANI MWEMA IKWIRIRI 3-4/12/2002**

**UTANGULIZI:**
Wilaya ya Kisarawe ni miongoni mwa wilaya sita zilizopo mkoani Pwani. Wilaya ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 3,535.

Wilaya imegawanyika katika Tarafa 4, Kata 14, vijiji 77 na Vitongoji 226. Wilaya iko umbali wa meta 1,000 toka usawa wa bahari wa kiwango cha joto, nyuzi joto 28-30. Kuna vipindi viwili vya mvua ambavyo ni vuli mwezi October hadi December na masika kuanzi Machi hadi Juni. Kiwango cha mvua kwa mwaka ni milimita 1000 – 1600.

### 4.11.1 Raslimali zilizopo Wilayani

- **Ardhi**
- **Misitu**
- **Wanyamapori**
- **Samaki – (mto Ruvu)**
- **Mazao ya Kilimo**
- **Madini (kaolin)**
- **Nyuki**

**Raslimali zipo kwenye ardhi kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.**

| MATUMIZI YA ARDHI | UKUBWA WA ENEO KM | ASILIMIA | SHUGHULI |
|---|---|---|---|
| Hifadhi ya misitu | 241.2 | 6.8 | Misitu ya Hifadhi ya Pugu, Kazimzubwi, Masanganya na Ruvu Kusini |
| Wanyamapori | 100 | 2.83 | Eneo linalozunguka hifadhi ya Selous |
| Kilimo | 380 | 10.7 | Mazao ya chakula na biashara |
| Makazi | 100 | 2.8 | Maeneo ya kuishi watu |
| Ufugaji na malisho | 310 | 8.8 | Eneo limetengwa Tarafa ya Mzenga na Chole |
| Maeneo ya Wazi (Umma) | 2,403.8 | 67.97 | Misitu, Vichaka, mabonde, Tambarare na mito. |
| JUMLA | 3,535 | 100% | |

**MADINI:**
KAOLIN – Inapatikana katika hifadhi ya msitu wa Pugu eneo la Mambisi. Mgodi wa Kaolin una eneo la ukubwa wa kilomita za ukubwa 5. Hifadhi ya Kaolin ni karibu tani milioni 2, maeneo mengine yenye Kaolin ni eneo la Dongojasi.

**Chumvi: -** Chumvi inapatikana katika bwawa la kidualo, Tarafa ya Mzenga Kata ya Kirui.
Udongo mwekundu – udongo huu unapatikana kwa wingi hivyo kuwezesha uanzishaji wa viwanda vya kutengeneza matofali (copressed bricks)

**Miradi inayosimamia mambo ya maliasili Wilayani Kisarawe ni kama ifuatavyo:**

| SEKTA | JINA LA MRADI | WANAOSAIDIA |
|---|---|---|
| Misitu | Hifadhi ya misitu ya Pugu na Kazimzumbwi | WCST – Wildlife Conservation Society of Tanzania<br>CARE – Misitu yetu |
| | Hifadhi ya misitu ya kijiji cha Kisanga | Wanakijiji wa Kisanga |
| | Hifadhi ya msitu wa Ruvu Kusini | CARE – Tanzania<br>TFCG – Tanzania Forest Conservation Group |
| Wanyamapori | Uhamasishaji wa wanakijiji katika utunzaji wanyamapori kando kando ya Hifadhi ya Selous (Kidunda, Vikumburu, Chole, na Kimalamisele) | Selous, Halmashauri na Idara ya Wanyamapori |

**2.0 Ukusanyaji Ushuru.**
Shughuli za ukusanyaji ushuru wa mazao ya Maliasili hufanywa kwa:

A) Kutoa leseni za mazao ya misitu na wanyamapori kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa.
B) Vijiji kukusanya ushuru wa Halmashauri kwa kutumia WEO na VEO kwa mazao ya misitu (HW5)

**3.0 Mikakati ya Wilaya dhidi ya matumizi haribifu ya maliasili.**
(a) Doria – Doria za mara kwa mara kwenye misitu ya Hifadhi na eneo la wazi.

- Doria za msimu kwa kushirikisha watumishi kutoka Wizara ya maliasili mf. Kikosi cha antipoaching.

(b) Kutoa elimu bora na endelevu ya mazao ya maliasili kwa kutumia watumishi waliopo na NGO's zinazohusika na maswala ya maliasili.

c) Kutunga sheria ndogo ya kuhifadhi mazingira.

**3.0 MASUALA YENYE UTATA**
(a) Hakuna alama kwenye ardhi zinazoonyesha mipaka ya Wilaya.

**4.0 MBINU ZA KUTATU**
(a) Wataalam wa ardhi wa pande zote wakishirikiana na Serikali za vijiji za mipakani kutembelea maeneo na kuweka alama zinazoonyesha mipaka ya Wilaya. Viongozi wa pande zote kuhamasisha wananchi kutunza na kuheshimu alama zilizowekwa.
(b) Sheria ambazo haziendi na wakati/sera

- **Sheria za misitu**
- **Wanyamapori**
- **Ardhi**

Kesi nyingi kuchukua muda mrefu mahakamani bila kutolewa hukumu au mashahidi kuitwa mahakamani (mf. Kesi za nyara).

### 4.11.2 MBINU ZA KUTATUA

Viongozi na wataalam mbalimbali watoe mapendekezo ya kuandaa miswada na kuwasilisha kwenye mamlaka husika kwa utekelezaji.

**5.0 Mbinu za pamoja ili kutatua matatizo yanaokwamisha juhudi za Wilaya katika kuhifadhi maliasili.**
a) Doria – Kwa kuwa na usafiri wa kuaminika kila wakati unapohitajika.
b) Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa njia mbali mbali kama vile:

- **Sinema**
- **Vijarida**
- **Mabango**
- **Semina mbali mbali na mikutano hasa kwenye vijiji vya mpakani**

## 6.0 MASUALA YA JINSIA NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Wanawake ndio watumiaji wakubwa wa nishati itokanayo na miti hivyo kuna haja kubwa ya kuwashirikisha kwenye hatua mbalimbali za kuhifadhi mazingira.

Hapa Wilayani Kisarawe wanawake wamechaguliwa kwa uwiano (Gender balance) za kuunda kamati za vijiji za kuhifadhi mazingira kwa mfano vijiji tisa vinavyozunguka hifadhi ya Pugu na Kazimzumbwi, (pamoja na kikundi cha WAHIPUKA) watetezi wa Hifadhi ya Pugu na Kazimzumbwi.

## 7.0 MTANDAO WA HABARI

Wilaya ya Kisarawe inayo Radio Call kupashana habari na vituo vyake ambavyo vipo:

- **Mzega**
- **Maneromango**
- **Chole**
- **Kisarawe Bomani**

Tuna imani endapo mtandao wa habari wa pamoja ukianzishwa utaongeza ushirikiano kati ya hizi Wilaya jirani.

## 4.12 Kiambatisho Namba. 12: Maelezo Ya Wilaya Ya Kisarawe Kuhusu Utoroshaji Wa Mazao YaMisitu Na Wanyama Kutoka Kisarawe

**SHA JUU YA UJIRANI MWEMA TAREHE 3-4/12/2002 IKWIRIRI**

Mazao ya misitu na wanyama yanatoroshwa Wilayani Kisarawe kupitia kwenye Wilaya zote za jirani. Wilaya hizo ni Ilala, Kibaha, Morogoro vijiji, Rufiji na Mkuranga.

Mazao mengi ya utoroshaji yanavunwa kwenye vijiji vya mpakani mwa Wilaya zilizotajwa hapo juu.

AINA ZA MAZAO.

**Mazao mbali mbali yanayovunwa ni pamoja na:-**

1. Magogo
2. Mbao
3. Nyara mbalimbali
4. Nyama (kitoweo)

Sababu za utoroshaji wa mazao ya maliasili:
(a) Kuwepa kulipa ushuru wa serikali kuu na ushuru wa Halmashauri
(b) Kukwepa kukaguliwa kwenye vizuizi vya Maliasili
(c) Uhaba wa watumishi wa kufanya doria za mara kwa mara.
(d) Uhaba wa vitendea kazi mfano magari, sare za kazi n.k.

**Maeneo ya utoroshaji wa mazao ya misitu na wanyama kwenye Wilaya za Kisarawe, Rufiji na Mkuranga ambazo ziko kwenye ukanda wa mashariki ni kama ifuatavyo:-**

**Wakati wa Kiangazi**
Magari kutoka Kihare, Makima, Chole na Vikumburu hubeba magogo, mbao, nyara na nyama ya pori kupitia Mloka hadi Mtanza – Rufiji.

**Wakati wa Masika**
Uvunaji kwenye maeneo ya Makima, Vikumburu, Chole na Kihare kwa wavunaji haramu unakuwa mkubwa kwa kubeba kwa baiskeli na kichwa kwa vile ubebaji wa kutumia magari unakuwa mgumu kutokana na mvua nyingi. Magari machache kupitia barabara ya Vikumburu Kisarawe kusafirishia mazao hayo.

Madhara ya utoroshaji wa mazao ya misitu na wanyamapori kutoka Wilaya moja hadi nyingine.

- Ukosefu wa mapato kwenye Wilaya inayoibiwa mazao yake.
- Uharibifu wa mazingira
- Uvunaji usiokuwa wa mpango.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**
(a) Kufanya doria usafiri unapopatikana
(b) Kuelimisha wafanyabiashara hasa wakati wa kutoa leseni na wakati wa ukaguzi kwenye vizuizi vya maliasili.
(c) Wahalifu huchukuliwa hatua za kisheria mara wapatikanapo aa uhalifu, mfano watu 21 walifikishwa mahakamani katika kipindi cha 2001 – 2002.

**SHUGHULI MUHIMU ZA USHIRIKIANO**

1. Kufanya mikutano ya pamoja na mialiko ya ujirani mwema.
2. Kufanya doria ya pamoja kushirikisha vijiji vya mpakani katika ulinzi

**Ms.Lilian Lukambuzi, NEMC, Dar es Salaam.**



**TOLEO MAALUM**

**Taarifa hii ya Warsha inakabidhiwa / inatolewa kwa heshima**

**ya kumkumbuka marehemu E.N. Mushi**

**aliyekuwa Afisa Misitu (W) Kisarawe.**

**Marehemu anakumbukwa**